MID WEEK JACKPOT!
TZS. 544,830,140
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Wafariki** ajalini wakisafirisha wahamiaji haramu

UKURASA 3




UKURASA 9


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Aprili 9, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581275

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




# Biashara ndizi za kwenye umeme ilivyoteka soko

UKURASA 2



Wananchi wakiwa katika pilikapilika za kununua mahitaji kwa ajili ya Sikukuu ya Pasaka katika Mtaa wa Congo, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Wamiliki malori walia ongezeko kodi ya mapato

UKURASA 2

MIAKA 59 YA MUUNGANO
TOLEO MAALUM
26TH APRIL
TANGANYIKA & ZANZIBAR



Kampuni ya the Guardian Limited, Wachapishaji wa Magazeti ya the Guardian na Nipashe, inawakaribisha wadau wote wa maendeleo kutoa salaam za pongezi wakati tunaadhimisha miaka 59 ya muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Toleo hili litachapishwa tarehe 26 Aprili, 2023 kwenye Magazeti ya Guardian na Nipashe.

The Guardian
Nipashe

Kwa mawasiliano zaidi,
Tupigie +255 677 020 701

Email: advertise@guardian.co.tz or Visit us at The Guardian Limited, Mikocheni Light Industrial Area, Opposite ITV / Radio One, Dar es Salaam
Web: www.ippmedia.com / epaper.ippmedia.com

# Polisi walivyofukua nyumba kusaka mwili wa mwanamke

UKURASA 3

MICHEZO SIMBA YATANGAZA OPERESHENI APRILI UK. 24
MAONI, KATUNI UK.6

# Wamiliki malori walia ongezeko la kodi

**Na Maulid Mmbaga**

CHAMA cha Wamiliki Wadogo na Wakubwa wa Malori Tanzania (TAMSTOA), kimelalamika kupandishwa kwa kodi ya mapato kwa asilimia 100 na kusema hali hiyo inawakandamiza na kushindwa kuendesha biashara zao.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa TAMSTOA, Chuki Shabani, alisema hali hiyo pia inasababisha wafanyabiashara wengi hususani wakubwa kuhamisha biashara zao katika mataifa mengine.

Alisema kwa sasa wanatakiwa kulipa Sh. milioni 2.7 kwa gari moja ikiwa ni gharama ya kodi kwa mwaka huku akiweka bayana kwamba kiwango hicho kinawakandamiza kibiashara.

Kutokana na hali hiyo, alishauri kushushwa hadi Sh. milioni moja na kwamba wamependekeza njia mbadala za ukusanyaji wa mapato ambazo zitaongeza kiwango cha ukusanyaji kodi bila kuathiri wafanyabiashara.

"Tunaiomba Wizara ya Fedha (na Mipango) kipitia Waziri Mwigulu Nchemba kama ameipata barua yetu, aijibu ili na sisi tuwajibu wasafirishaji wajue nini kinachoendelea kwa sababu mpaka sasa hawaelewi kitu gani kinaendelea.

"Watu wengi wenye uwezo wamehamisha biashara zao nchini kitu ambacho ni kibaya kwa uchumi wa nchi yetu. Sasa tunaomba kabla wengine hawajaikimbia nchi, ni vizuri tukakaa tukafikia mwafaka nini kifanyike ili kuondokana na tatizo hili," alisema.

Aidha, alimwomba Rais Samia Suluhu Hassan awasikilize kwa kuwa nia yao ni kujenga na kufikia malengo ambayo serikali imejiwekea bila kumuumiza mtu.

Pia alibainisha kuwa Tanzania kuna kodi nyingi ambazo hazikusanywi kupitia magari, hivyo akishauri kuwa serikali inaweza kukusanya kodi kupitia uchafuzi wa mazingira kutokana na moshi unaotokana na mafuta ya petroli za magari.

Alishauri kuwa endapo kikiwekwa kiwango cha Sh. milioni moja, kusingekuwapo na wafanyabiashara kukimbilia nchi za jirani, kwamba wangefanya usajili wa magari yao hapa nchini.

Kadhalika, alibainisha kuwa wanaunga mkono mchakato wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) wa kuwasajili madereva wa malori, licha ya kudai kuwa utaratibu na vigezo vilivyowekwa siyo rafiki kwa wahusika na kwamba inasababisha wengi kushindwa kusajiliwa.

Alishauri LATRA itumie namba za leseni za udereva kuwasajili madereva husika badala ya kuhitaji cheti ambacho kutokana na mazingira yao siyo rahisi kila mmoja kuwa nacho kwa sasa.

Pia aliishukuru serikali kwa kuwaunga mkono katika safari ya kwenda kutatua tatizo la foleni katika mipaka ya Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), akieleza kuwa walipata ushirikiano kutoka kwa nchi hizo na kufanikiwa kumaliza tatizo.



Mchuuzi akionyesha ndizi zenye mwonekano wa njano zilizoivishwa kwa mashine maalum inayotumia umeme. **PICHA: JENIFER GILLA**

# Biashara ndizi za kwenye umeme ilivyoteka soko Dar

**Na Jenifer Gilla**

UKISTAAJABU ya Musa utaona ya firauni. Ndivyo unavyoweza kusema baada ya soko la ndizi mbivu zilizoivishwa kwa kutumia teknolojia ya umeme kutawala jijini Dar es Salaam.

Nipashe ilitembelea maeneo yalipo makontena yanayotumika kuivisha ndizi hizo ikiwamo Tabata, Msimbazi Center na Gongo la Mboto na kuzungumza na wanaohusika na biashara hiyo.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Mariam Mbaraka kutoka Tabata, alisema asilimia kubwa ya ndizi mbivu zilizoko sokoni kwa sasa zinaivishwa kwa umeme na hiyo imetokana na ubora na mvuto uliopo katika bidhaa hiyo.

Alisema ubora huo unatokana na namna ndizi hizo zinavyoivishwa kwa kuwekwa kwenye makontena ya kuhifadhia samaki wabichi, yenye baridi kwa siku tatu kwa ajili ya kulifanya ganda la nje liwe gumu ili ndizi hizo zisiharibike haraka.

Mbaraka alisimulia kuwa baada ya siku tatu kupita wanaziwekea gesi au majiko ya moto ili zipate joto na kuiva, shughuli inayofanyika kwa siku moja, zikishaiva wanaziwashia feni kwa siku moja kwa ajili ya kuleta rangi ya njano.

"Kwa hiyo ni shughuli inayochukua takribani siku nne mpaka kuwa tayari. Kwa ufupi tumeboresha njia ya kuivisha ndizi baada ya kuona njia ya asili haileti matokeo mazuri kutokana na joto kuongezeka," alisema.

Baada ya ndizi hizo kuiva, alisema anazipeleka sokoni ambako anaziuza kwa jumla kwa bei ya Sh. 150 hadi 200 kulingana na ukubwa wa ndizi huku kontena moja lenye maboksi 600 ya ndizi anaziuza kwa siku mbili hadi tatu, hivyo kupata takribani Sh. milioni 12.

Mbaraka ambaye awali alikuwa akiuza ndizi kwa bei ya rejareja, alisema kilichomvutia kuingia katika biashara hiyo ni namna ndizi hizo zinavyonunuliwa na watu kulinganisha na zilizoivishwa kwa njia ya asili.

"Yaani hizi ndizi zikishushwa pale sokoni mpaka ziishe ndipo hawa walioivisha kwa njia ya asili wanapata wateja. Kwa hiyo niliona kuna faida, hivyo nikatafuta watu wakaniunganisha na wanaokodisha haya makontena nami nikaanza kazi. Kipindi hicho naanza (mwaka 2016) waivishaji walikuwa si wengi kama sasa," alisema.

Kwa mujibu wa Mbaraka, teknolojia hiyo ililetwa nchini na raia wa Ujerumani aliyetokea Kenya lakini baada ya muda alifunga biashara hiyo na kurudi kwao ndipo wafanyakazi wake wa Kitanzania wakaiiga na kuja kufundisha wengine.

Sebastian Mgaya, mfanyabiashara mwingine kutoka Msimbazi Center alisema alianza biashara hiyo kwa kukodisha kontena moja mwaka 2017 na sasa ana makontena matatu kutokana na kukua kwa soko siku hadi siku.

Alisema wanachofanya ni kugeuza uivishaji ndizi wa njia ya asili kwa kutumia teknolojia kwa kuwa njia ya zamani haileti matokeo mazuri kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

Alisema hapo zamani mtu alikuwa anaweza kuweka ndizi kwenye sakafu ili ipate ubaridi kwa ajili ya kuimarisha ganda la juu na isiive kwa siku mbili lakini sasa hivi haiwezekani kutokana na joto kuwa kali matokeo yake ndizi inaiva ikiwa na rangi ya kijani na uchachu.

"Ndizi iliyo bora na tamu inatakiwa uivishaji wake upitie steji tatu, kuimarisha ganda, kuiivisha na kisha kuiweka nje ipigwe na upepo ili iwe ya njano. Sasa hivi joto ni kali ndizi zinaiva haraka kwa hiyo tunashukuru kupata hii teknolojia" alisema.

Rosemary James, mfanyabiashara wa bidhaa hiyo kwa rejareja Tabata Relini, alisema tangu alipoanza kuuza ndizi hizo mwaka 2018, ameona matokeo makubwa ikilinganishwa na zinazoivishwa kiasili.

"Zile ndizi za zamani (za asili) ilikuwa ukinunua unatakiwa uuze ziishe, zikilala tu zinaoza. Kwa hiyo kwa siku nilikuwa napata hasara hadi ya Sh.3,000 lakini hizi zinakaa hadi siku tatu. Lakini pia hizi rangi yake ina mvuto, mtu akiona zinamshawishi kununua tofauti na zile za zamani zilikuwa na rangi ya kijani na madoa," alisema.

**USALAMA JE?**

Ofisa Kilimo kutoka Wizara ya Kilimo, George Boki, aliithibitishia Nipashe kuwa wanaifahamu njia hiyo na kuwa ni moja ya njia salama za kuivisha ndizi kisasa.

Alisema hawana wasiwasi na njia hiyo kwa kuwa mpaka sasa hawajapokea malalamiko yoyote juu ya usalama wa njia hiyo kutoka kwa wadau wa usalama wa chakula likiwamo Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

"Tumekuwa tukitoa elimu juu ya njia mbalimbali za kuivisha ndizi mbivu zikiwamo za kisasa na za kienyeji, hii njia tunaifahamu, ni moja ya njia bora ya kuivisha ndizi kisasa, na nzuri kwa wafanyabiashara. Kuhusu malalamiko ya usalama hatujasikia labda TBS wao ndio watuambie," alisema George.


## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**BAKARI ALI BANGU** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 349 AHU – LAYLAND.** Kadi ya gari yenye namba za usajili **T 899 ARB – FIAT.** Kadi ya gari yenye namba za usajili **T 432 BTA – TRAILER.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/123903/2023.**



**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY**
**Notice of Appointment of Liquidator: Voluntary Winding- Up: for insertion in Gazette pursuant to section 360 of the companies Act 2002**

**Company Number** 56941

**Company Name (In full)**
THE GUINEA COMPANY DECORATION AND DESIGNS LIMITED

**Type of Liquidation** MEMBERS

**Address of Registered office**
REGION ARUSHA, DISTRICT ARUMERU, WARD USA RIVER,POSTAL CODE 23301 STRET NGARESERO ROAD BIASHARA RD, PLOT NUMBER 255, 257 BLOCK A, HOUSE NUMBER 255,257

**Liquidator(s) Name(s)** MATUBA NYEREMBE
**Liquidators(s) Address(es)** KANISANI ROAD P.O.BOX 1947 ARUSHA

**Date of appointment** 10-3-2023
**By whom appointed** DIRECTORS

Signed...................... Date....................

NAME IN BLOCK LETTERS.........MATUBA NYEREMBE
*(by each liquidator if more than one)*

**Signed**..............................Date............................

NAME IN BLOCK LETTERS....................................



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya UBUNGO**

**Kituo cha JUMUISHI TEMEKE Mkoa DAR ES SALAAM**

**Usimamizi wa mirathi Na 540/2023**

**KATIKA MAHAKAMA INAYOTEMBEA KIBAMBA**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU HALIDI JUMA LUSEKO WA SINZA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA MARGARET NAMBUYA LUSEKO**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 18 mwezi 04 mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Imetolewa leo tarehe 04 mwezi 04 mwaka 2023

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
KIMARA KINONDONI

HABARI KITAIFA

# Polisi walivyofukua nyumba kusaka mwili wa mwanamke

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Polisi mkoani Geita limelazimika kufukua ndani ya nyumba ya mwalimu wa Shule ya Msingi Lubanga, Francis Elizeus, baada ya ndugu wa mke wake kumtuhumu kuwa amemuua mke wake, Jennifer Mashimo, na kumfukia ndani.

Inadaiwa kuwa Jennifer alikuwa na tabia za kutoweka nyumbani kwa zaidi ya mwezi mmoja lakini tangu alivyotoweka Machi 2020, hajarudi hali iliyosababisha wanafamilia kuwa na shaka na mume wake.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Geita, Kamishna Msaidizi (ACP) Safia Jongo, alisema walipata taarifa ya tukio hilo, wakafuatilia kibali cha Mahakama ili kujiridhisha juu ya uwapo wa mwili ndani ya nyumba ya wanandoa hao. Hata hivyo, walipoingia ndani ya nyumba hiyo hawakuupata.

"Aprili 3, mwaka huu, tulipata kibali tukaanza kufukua, tulifanikiwa kufukua mashimo manne yaliyokuwa yanahisiwa na ndugu hao.

Mpaka inafika usiku hatukupata matokeo yoyote. Tukarudi Aprili 5 na kufukua maeneo yaliyokuwa yanashukiwa kadhalika hatukuupata mwili wa mwanamke huyo. Kwa hiyo familia na wenyewe wakathibitisha kwamba hakuna mwili uliofukiwa," alisema Jongo.

Kamanda Jongo alisema kwa sababu za kiuchunguzi na usalama, imewalazimu kumshikilia mwalimu huyo ili kumwepusha na watu wanaomtishia maisha.

"Tunahofia usalama wake kwahiyo uchunguzi utakapokamilika wale ambao wanatishia usalama tutawachukulia hatua lakini huyu mwalimu bado tunamhifadhi kwa ajili ya usalama wake", alisema Jongo.

Aidha, Kamanda Jongo alisema kutokana na jeshi hilo kupokea taarifa hizo rasmi, watafanya utaratibu wa kuendelea kumtafuta kwa kuzitangaza picha zake kwenye kwenye vyombo vya habari ili kama bado yuko hai na yuko mahali kupatikana na hatua zaidi zichukuliwe.

Kwa mujibu wa Kamanda Jongo, walimhoji mama wa Jennifer ambaye alikiri kwamba mtoto wake alikuwa na tabia ya kuondoka nyumbani akigombana na mume wake na kurudi baada ya mwezi au miezi mitatu.

Alisema lakini imekuwa tofauti kwa kipindi hiki kwa kuwa tangu aondoke Machi 2020, hakuwahi kurudi hali iliyosababisha ndugu hao kuhisi mtoto wao ameuawa na mume wake na kuzikwa ndani ya nyumba.

# Wafariki dunia kwa ajali wakisafirisha wahamiaji

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WATU wawili wanaodaiwa kuhusika katika kusafirisha wahamiaji haramu, wamefariki dunia baada ya gari walilokuwamo kugongwa na lori lililokuwa limebeba wahamiaji hao.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Hamisi Issah, alisema hayo jana kuwa ajali hiyo ilitokea juzi majira ya saa 9:00 usiku katika Kijiji cha Mng'elenge wilayani Wanging'ombe.

Alisema watu hao waliofariki dunia walikuwa katika gari dogo lenye namba za usajili T957 DCL Toyota Mark X ambalo liligongwa na lori lenye namba T 497 BTE aina ya Scania ambalo lilikuwa limewabeba wahamiaji hao.

"Kulitokea ajali kati ya lori na gari moja aina ya Mark X wale waliokuwa kwenye gari dogo walifariki dunia wote," alisema Kamanda Issah

Kamishna wa Uhamiaji Mkoa wa Njombe, Vincent Haule, alisema walifanya msako katika mashamba baada ya kupata taarifa kutoka kwa wananchi kwamba waliwaona wahamiaji hao waliokuwa wakijificha baada ya kunusurika kwenye ajali.

Alisema baada ya kufanya msako, Jeshi la Uhamiaji lilifanikiwa kuwakamata wahamiaji haramu 63 ambao walikuwa wamejificha katika mashamba.

"Hawa wahamiaji walikuwa wametoka Nairobi nchini Kenya wakafika Mombasa na kuingia mkoani Tanga. Tumeshawapata 63 bado wengine kama 40 wanaendelea kutafutwa. Tuombe wananchi mtakapowaona raia kama hawa wa Ethiopia mtupe taarifa," alisema Haule.

Akizungumza na Nipashe, mmoja wa wakazi wa wilaya ya Wanging'ombe, Tegemea Mahenge, alisema walisikia mlio wa ajali usiku wa manane.

Alisema walipofika eneo la tukio walikuta kumetokea ajali na kwamba watu waliokuwa kwenye gari dogo mmoja alikuwa amefariki dunia, huku wahamiaji haramu ambao walijificha katika mashamba walikuwa na hali mbaya kiafya na kuanza kuwapa huduma ya kwanza.

Diwani wa Wanging'ombe, Geofrey Nyagawa, na Mtendaji wa Kijiji cha Mng'elenge walizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, waliwataka wananchi kujiepusha na biashara haramu kwa kuwa athari zake ni kubwa.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
09.04.2023

TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Jumatano tarehe **19-04-2023** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port kuelekea Rufiji,** gari hizoo zina namba za usajili: **T 660 BZU / T 387 DHQ T 985 DTN / T 416 AYQ T 903 DSD / T 499 DZX T 807 DYL / T 310 DDH**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 22.00**
   **Upana - mita 7.47**
   **Kimo - mita 4.70**

2. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, Pwani hadi Rufiji** kupitia Kibiti

3. Gari itasafiri muda wa usiku ***(Kuanzia saa 08:00 usiku mpaka saa 11:00 alfajiri)*** kutoka **Dar es salaam port, pwani mpaka Kibiti.** Kutoka Kibiti kwenda Rufiji gari itasafiri muda wa mchana ***( kuanzia 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

217361902



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
09.04.2023

TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya 11-04-2023 kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port kuelekea Kilombero kupitia Mikumi,** gari hizo zina namba za usajili: **T 203 DYJ / T 837 DJB T 204 DYJ / T 273 DUH T 653 DFA / T 630 AJA T 118 EAG / T 877 EAU**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 21.00**
   **Upana - mita 4.20**
   **Kimo - mita 5.23**

2. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, hadi Kilombero kupitia Mikumi,** gari itasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

217361702



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
09.04.2023

TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Jumatano tarehe 19-04-2023 kampuni ya Mainline Carriers Ltd itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka Dar-Es-Salaam Port kuelekea Rufiji, gari hizo zina namba za usajili:
   **T 687 DUB / T 394 DVS T 163 DFC / T 393 DVS**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 22.00**
   **Upana - mita 5.20**
   **Kimo - mita 4.60**

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, Pwani hadi Rufiji kupitia Kibiti,** gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

217361802



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akimfariji, Anna Mushi (kulia), ambaye ni mama wa marehemu, Faithnancy Mwanjile, alipohani msiba huo nyumbani kwa Brig. Jen Mstaafu Aloyce Mwanjile, Bunju mkoani Dar es salaam jana. Katikati ni mke wa Waziri Mkuu, Mary Majaliwa. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Watu saba mbaroni tuhuma za mauaji

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

WATU saba wamefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Manyoni mkoani Singida wakikabiliwa na shtaka la mauaji.

Washtakiwa hao ni Othman Khamis, Shaban Mussa, Mussa Swedi, Omary Jumanne, Hamim Yahaya, Salum Ibrahimu na Oscar Issa.

Mwendesha Mashtaka, Mkaguzi Msaidizi Ryoba Mkambala, akisoma shtaka hilo mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Felician Kapama, alidai washtakiwa wote kwa pamoja usiku wa Machi 3, mwaka huu, walimuua mtu mmoja ambaye hakufahamika jina lake, anayekadiriwa kuwa na umri wa kati ya miaka 40 na 45.

Alidai kuwa washtakiwa hao wametenda kosa hilo la mauaji kinyume cha kifungu 196 na 197 vya Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16.

Hata hivyo, washtakiwa hao hawakutakiwa kujibu lolote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo ambapo upelelezi bado unaendelea.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Aprili 18, mwaka huu, huku washtakiwa wakipelekwa mahabusu.

Wiki iliyopita, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Stella Mutabihirwa, alitangaza kukamatwa kwa watu sita ambao wanatuhumiwa kujihusisha na vitendo vya mauaji ya watu na kufukua makaburi wilayani Manyoni.

Kamanda Mutabihirwa alisema watu hao walikuwa wakichukua sehemu za siri za watu waliozikwa kwa ajili ya kutengeneza dawa ya kupata utajiri, kuwauzia wateja wao.

Alisema watuhumiwa hao walikamatwa baada ya msako uliofanywa na Jeshi la Polisi kuanzia Machi 16 hadi 24, mwaka huu, katika maeneo mbalimbali wilayani Manyoni na vijiji jirani vya wilaya ya Sikonge mkoani Tabora.

Alisema watuhumiwa hao baada ya kukamatwa na kuhojiwa walikiri kuhusika na mauaji ya mtu mmoja mwanamume ambaye hajafahamika jina lake mwenye umri kati ya miaka 40 na 45 eneo la Relini Manyoni, huku kifo chake kikisadikiwa kilitokana na kukanyagwa na treni.

Kamanda Mutabihirwa alisema baadhi ya viungo vya mtu huyo vilikuwa pembeni katika njia ya treni, huku viungo vya sehemu za siri vimenyofolewa.

"Tulivyowahoji watuhumiwa walikiri kuhusika na tukio hilo na kueleza kwamba walikata sehemu za siri kama nywele, kucha na ulimi kwa lengo la kutengeneza dawa ili kuwapatia wateja wao wanaohitaji utajiri," alisema.

Aliongeza kuwa watuhumiwa hao pia walikiri kujihusisha na vitendo vya kufukua makaburi wilayani Manyoni na kuua watu kwa lengo la kupata viungo vya binadamu kwa ajili ya kutengeneza dawa ya kupata utajiri.

# Wakristo wakumbushwa kuwa na moyo wa huruma

**Na Steven William,** MUHEZA

Mchungaji Kiongozi wa KKKT Usharika wa Muheza Mjini mkoani Tanga, John Ndimbo, amewataka waumini wa kanisa hilo kuwa na moyo wa huruma hasa katika kipindi cha mateso na kufufuka kwa Yesu Kristo.

Akihubiri wakati wa ibada ya Ijumaa Kuu iliyofanyika juzi katika kanisa hilo, Mchungaji Ndimbo aliwataka waumini wawe tayari kusamehe kwa wote waliowakosea na kuondoa visasi na vinyongo ambavyo vinaweza kuharibu maisha yao.

"Katika kipindi hiki cha kukumbuka mateso ya Yesu Kristo, tunapaswa kukumbuka matendo ya huruma ambayo yatazidi kutuongezea imani na kuondoa visasi na malumbano katika jamii na familia zetu," alisema.

Aidha, aliwataka wakristo kujifunza kukaa kimya ili kuepusha maneno na kumgeukia Yesu ili waweze kumweleza shida zao, jambo ambalo alisema linaweza kuwasaidia wakikutana na huruma yake.

Mchungaji huyo pia alimtaka kila mmoja kuweka azimio la kuwa mtetezi kwa wanaoonewa na kamwe wasinyanyase mtu au kumtendea mabaya.

Alisema katika ngazi ya familia lazima kuwe na roho ya msamaha ili kudumisha amani na utulivu ikiambatana na kuombea amani nchini na Rais Samia Suluhu Hassan ili kusitokee machafuko.

"KKKT tunatakiwa palipo na chuki tulete mapendo, palipo na kukosewa tulete msamaha na palipo na giza tulete nuru, maana sisi ni watoto wa Kristo," alisema mchungaji huyo.

Aliongeza: "Waliomsulubisha Yesu msalabani walikosa maarifa na ukikosa maarifa ya Mungu unakuwa mtu unayekwenda kichwa kichwa. Watu wale walikosa maarifa ya kujua Yesu ni nani.

"Walijawa hofu wakidhani Yesu ataleta mapinduzi katika shughuli zao, kukosa maarifa kwao ni sababu moja iliyomuua Yesu. Pia hofu na woga wa kutokuwa tayari kuusimamia ukweli miongoni mwao".

# Waziri aonya atakayejaribu kuuza madume yaliyotolewa na serikali

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amekabidhi madume bora 40 ya ng'ombe kwa vikundi vya wafugaji wilayani Mkalama mkoani Singida huku akionya atakayedhubutu kuuza ng'ombe hao kipindi hiki cha sikukuu atakuwa anajitafutia kesi ya uhujumu uchumi.

Akikabidhi ng'ombe hao wiki hii katika hafla iliyofanyika kijiji cha Iguguno wilayani hapa, alisema serikali imenunua madume ya ng'ombe 366 kwa thamani ya zaidi ya Sh. milioni 878.4 ambao watagawiwa wafugaji kwenye halmashauri nane nchini.

"Isitokee mtu haya madume akachinja kwa ajili ya sikukuu. DC (Mkuu wa Wilaya) huyo atakayefanya hivyo usimwache kwanza atakuwa anajitafutia kesi ya uhujumu uchumi ambayo haina dhamana," alisema.

Ulega alisema baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kufungua milango, nchi nyingi zimekuwa zikihitaji nyama kutoka Tanzania lakini bahati mbaya ng'ombe wa asili wanaofugwa na wafugaji hapa nchini hawana uzito nyingi zinakuwa kati ya kilo 80 hadi 120 tu.

Alisema madume bora ya ng'ombe ambayo yamenunuliwa na serikali watoto watakaozaliwa wa Zebra na Boran watakuwa na uzito wa kati ya kilo 150 hadi 200 na ubora unaotakiwa.

Pia Ulega aliwataka wafugaji nchini kuachana na fikra za kuwa na makundi makubwa ya mifugo ambayo mingi inaishia kufa kwa ukame na badala yake wawe na utaratibu wa kuivuna na kuiuza ili kuimarisha kipato chao na kuepukana na hasara zinazoweza kuzuilika.

Alisema wafugaji wabadilike waachane na ufugaji kama wa enzi za mababu zetu wa kuwa na makundi mengi ya ng'ombe ambao inapotokea ukame wanakufa na kusababisha hasara kwa mfugaji.

Aliongeza kuwa wafugaji waanze kumiliki maeneo yao kwa ajili ya malisho na halmashauri zihakikishe wafugaji ambao wana maeneo ya malisho wanapimiwa na kupewa hati ili kuepusha migogoro ambayo imekuwa ikijitokeza kati ya wakulima na wafugaji.

Mkurugenzi Msaidizi Uzalishaji Mifugo kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Simon Lyimo, alisema serikali imenunua madume bora ya ng'ombe ambayo yamesambazwa kwenye halmashauri za Mkalama ambayo imepewa madume 40, Msalala (50), Chato (50), Maswa (50), Chamwino (50), Buchosa (46), Mvomero 40 na Mkuranga 50.

Lyimo alisema serikali imenunua madume hayo ikiwa ni mpango wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika mabadiliko ya sekta mifugo ambayo pamoja na mambo mengine inalenga kuboresha mbari za mifugo ili kuwa na mifugo yenye tija zaidi.

Ofisa Mifugo Wilaya ya Mkalama, Joseph Michael, alisema madume hayo 40 yatagawiwa kwa kila kikundi dume mmoja na atatumika kwa wanakikundi wote ambapo kikundi kitawajibika kumtunza, kumlisha na matibabu ili kulinda ubora na ufanisi wake.

# CCM yaahidi kumaliza kero zinazowasumbua wananchi

**Na Is-haka Omar,** PEMBA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, kimesema kitaendeleza utamaduni wake wa kutekeleza ahadi zake kwa vitendo kwa nia ya kumaliza changamoto mbalimbali zinazowakabili wananchi.

Katibu wa Kamati Maalum ya NEC, Idara ya Itikadi na Uenezi, Khamis Mbeto Khamis, alisema hayo juzi wakati akikabidhi mashine ya maji safi na salama kwa wananchi wa kijiji cha Kangagani wilaya ya Wete kisiwani Pemba, Suleiman Ali Suleiman.

Alisema dhamira ya CCM ni kuendelea kusimamia kikamilifu utekelezaji wa ilani yake ya uchaguzi ya mwaka 2020-2025 kwa kuhakikisha changamoto ya tatizo la ukosefu wa maji safi na salama inamalizwa nchini.

Mbeto alisema mashine hiyo ya maji imetolewa na Naibu Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Mohammed Said Mohammed, ikiwa ni utekelezaji wa ahadi yake aliyotoa hivi karibuni aliposhiriki dua maalum ya kuiombea amani nchi.

Katibu huyo wa NEC alisema maji safi ni muhimu katika maisha ya kila siku ya mwanadamu, hivyo serikali kupitia taasisi zake zinazosimamia upatikanaji wa huduma hiyo ziongeze juhudi za kutatua changamoto hiyo.

"Chama Cha Mapinduzi Ofisi Kuu ya Zanzibar leo (juzi) tunakabidhi mashine hii ya maji safi na salama ili kuwaondolea usumbufu wa ukosefu wa maji katika kijiji hiki," alisema.

"Pia Naibu Katibu Mkuu, Dk. Dimwa kanielekeza niwaambie kuwa mwendelee kukiamini chama na serikali zake mbili huku mkidumisha amani, upendo na mshikamano," alisema.

Katibu huyo alishiriki katika hafla ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar na Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM, Hemed Suleiman Abdulla, aliyekabidhi futari kwa watumishi wa CCM wa mkoa wa Kusini Pemba.

Akizungumza mara baada ya kukabidhi futari hiyo, Hemed alisema ametoa sadaka hiyo kwa watumishi wa chama na ataendelea kutoa kwa mikoa mingine ili wapate futari ya uhakika katika mwezi huu wa Ramadhani.

"Nipo katika ziara yangu ya kiserikali ya kutembelea maeneo mbalimbali na kujumuika na waumini na wananchi wenzangu wa Pemba, lakini nikaona kuna umuhimu wa kutoa sadaka ndogo kwa watumishi wa CCM wa mkoa huu ambao ni 47. Kila mtumishi atapata kilo 25 ili ziwasaidie katika kipindi hiki cha mwezi wa Ramadhani.", alisema Hemed.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kusini Pemba, Yussuf Ali Juma, alimshukuru Hemed kwa uamuzi wake wa kuwasaidia watendaji wa CCM katika mkoa huo na kwamba hatua hiyo itaongeza ari ya juhudi za kufanya kazi kwa ufanisi.




Mwenyekiti wa Chama cha Wamiliki wa Malori Makubwa na Madogo Tanzania (TAMSTOA), Chuki Shabani (katikati), akiwasilisha taarifa ya mwenendo wa usafirishaji nchini, huku akiipongeza serikali kwa kuwaunga mkono katika safari ya kwenda kutatua changamoto ya foleni katika mpaka wa Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na kwamba wamefanikiwa kufikia muafaka, alitoa pongezi hizo jana mkoani Dar es Salaam. **PICHA:MAULID MMBAGA**

# Jafo: Upandaji miti uambatane na usimamizi wa mazingira na maadili

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, amesema wakati umefika sasa wa kuhamasisha kusimamia mazingira pamoja na maadili ili yasimomonyoke na kuleta athari kubwa nchini.

Jafo alisema hayo jana kwenye uzinduzi wa upandaji zaidi ya miti 35,000 uliojulikana kama kampeni ya Aprili ya Kijani ulioandaliwa na Kanisa la Kiinjili na Kilutheri Tanzania (KKKT) uliofanyika katika Usharika wa Mlimakola Dayosisi ya Morogoro.

Alisema licha ya kuwapo kwa uharibifu mkubwa wa mazingira nchini, kwa sasa kumekuwa na mmomonyoko mkubwa wa maadili ambao haupaswi kufumbiwa macho.

Kwa sasa, alisema kuna changamoto kubwa ya kumomonyoka kwa maadili na watu wanaotaka kuyamomonyoa hufanya kwa makusudi kwa kutumia fedha na mbinu mbalimbali.

Alisema katika hilo viongozi wa dini hawapaswi kuonea aibu suala zima la kulinda maadili ya mtanzania sababu wanapaswa kuyalinda bila kuchoka kwa kuzungumza na waamini wao na jamii kwa ujumla.

"Nchi haiwezi kuendelea bila kuwa na maadili mazuri hivyo niwaombe viongozi wa dini msione aibu wala msichoke bali tulinde maadili yetu kwa pamoja" alisema.

Dk. Jafo alisema athari za mabadiliko ya tabia nchi ni joto kuongezeka duniani na barafu kuyeyuka na kufanya kuongezeka kiwango cha maji jambo linaloashiria kupotea baadhi ya visiwa vidogo vilivyopo nchini kama vile hali inavyojitokeza katika sehemu ya kisiwa cha Pemba.

Alisema fahari ya Mlima Kilimanjaro pia inakuwa hatarini kwa sababu hivi sasa joto ni nyuzi 32 mkoani humo wakati inajulikana kuwa mkoa huo ni mji wa baridi mambo ambayo yanasababishwa na mabadiliko ya tabianchi.

Kwa mujibu wa Jafo, athari ya mabadiliko ya tabianchi bado ni kubwa nchini kwa sababu uchumi wa nchi unashuka, viwanda kushindwa kufanya kazi kwa kukosa maji na umeme, kilimo kushuka kwa kukosa mvua, mifugo kufa kwa kukosa maji na uchumi kuporomoka. Aliagiza ulinzi na utunzaji wa mazingira kwa kupanda miti na kuilinda uzingatiwe.

Aidha, Waziri Jafo aliwaomba watanzania kuwaunga mkono wadau wa mazingira katika suala zima la utunzaji wa mazingira kwa kuacha kuchoma misitu kwa kuwa wakifanya hivyo wanaharibu nchi.

"Kuhifadhi mazingira hakuchagui mtu, dini wala kabila. Sote tuna kila sababu ya kuhakikisha tunapambana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Ukienda kwa ndugu zetu walioko wilaya za Longido, Kiteto na Simanjiro mikoa ya Manyara na Arusha, mabadiliko ya tabianchi kule yameathiri zaidi.

"Unakuta mfugaji anapoteza mifugo hata 10 hadi 20 kwa siku huku anaona. Ukame umeshamiri wanyama wanakula mpaka udongo bahati nzuri tu mvua chache zilizonyesha siku za karibuni. Kuna watu wamekuwa maskini, kutoka kuwa matajiri wa mifugo mingi wamekuwa fukara kabisa, yote ni athari za mabadiliko ya tabianchi" alisema.

Jafo alihimiza masuala ya amani ya nchi kuendelea kulindwa ambayo ndiyo msingi wa ujenzi wa maendeleo ya nchi ikiwemo miradi mikubwa kama vile wa reli ya SGR na Bwawa la Mwalimu Nyerere.

Awali, Askofu wa KKKT Dayosisi ya Morogoro, Jacob Ole-Mameo, aliitaka jamii kutambua kuwa uhifadhi na utunzaji wa mazingira ndio uhai na maisha ya mwanadamu.

Alisema jamii inapaswa kutambua kuwa uharibifu wa mazingira ni jambo linalochangia mwanadamu kupoteza uhai wake kwa asilimia kubwa kwa sababu mazingira yanapoharibika mwanadamu atakosa mahitaji muhimu ikiwemo maji, hewa nzuri na chakula na hivyo kutishia uhai wao.

Hivyo alisema jamii inapaswa kuzingatia utunzaji mazingira na kuyafanya kubaki kama yalivyokuwa wakati mwana Adamu na Eva walivyoachwa na Mungu kwenye bustani ya Edeni ili waweze kuishi.

Meneja wa Shirika la Kikristo la Kuhudumia Wakimbizi Tanzania (TCRS) Mkoa wa Morogoro, Rehema Samuel, alisema kwa kushirikiana na KKKT na wafadhili wao, FELM, wamejipanga kupanda zaidi ya miti 35,000 katika maeneo mbalimbali nchini.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Pasaka iwe mwendelezo kutenda mambo mema

**LEO** ni Sikukuu ya Pasaka. Ni siku ambayo Wakristo duniani kote, husherehekea na kukumbuka kufufuka kwa Mwokozi wao Yesu Kristo yapata miaka 2,000 iliyopita.

Sikukuu hii pia ni hitimisho la mfungo wa siku 40 wa Kwaresma, muda ambao wenye imani ya dini hiyo, hutumia kufunga na kutafakari mafumbo mbalimbali ya imani ambayo huambatana na ibada za kila Jumatano za Kwaresma pamoja na ibada za Njia ya Msalaba kila Ijumaa kwa baadhi ya madhehebu.

Katika kusherehekea Pasaka, waumini hufurika katika nyumba za ibada kwa ajili ya mashangilio na kupokea mafundisho kutoka kwa viongozi wao kuhusu ufufuko na namna ya kuyaishi maisha ya ukristo. Ibada za Pasaka hutamatika siku ya Jumatatu zikiwa na ujumbe wa kutembea na Yesu Mfufuka.

Licha ya kuwapo kwa ibada katika makanisa mbalimbali, sikukuu ya Pasaka pia husherehekewa kwa vyakula na vinywaji ambavyo huandaliwa katika familia na baadhi ya watu hualika ndugu, jamaa na marafiki. Wakati mwingine, Pasaka katika baadhi ya familia hutumika kuwakusanya ndugu pamoja na kama kuna tofauti, basi huziondoa kutokana na mikusanyiko hiyo ya kifamilia.

Mbali na hayo, baadhi ya watu hukusanyika katika nyumba na maeneo ya starehe kwa ajili ya kuburudika kwa muziki, vyakula na vinywaji ikiwa ni shamrashamra za kukumbuka kufufuka kwa Yesu Kristo.

Katika eneo hilo, si Wakristo pekee ambao hukutanika bali waumini wa dini mbalimbali kama ilivyo kwa utamaduni wa Watanzania kuungana na kuburudika pamoja bila kujali rangi, imani wala itikadi. Kwa Dar es Salaam, baadhi ya watu huenda kwenye sehemu za starehe kama ufukweni wakiwa wameambatana na marafiki na wapenzi wao.

Pamoja na hayo, wahenga wanasema jambo lolote likizidi mipaka huwa majanga kwa baadhi, hivyo ni rai kwamba watu wanaposherehekea sikukuu hii, ni vyema wakaadhimisha siku hii kwa amani na utulivu na kufanya kila kitu kwa kiasi. Watu waache kutumia vilevi kupita kiasi pamoja na kuendesha vyombo vya moto kwa fujo na hatimaye kuhatarisha maisha yao na ya wengine.

Sambamba na hilo, ni vyema wan anchi, hususan waumini wa dini ya Kikristo, wanapaswa kuitumia sikukuu hii kwa kutafakari mambo waliyojifunza wakati wa kipindi cha Kwaresma. Katika kipindi hicho, baadhi ya watu hufunga kula au kujizuia baadhi ya vitu ambavyo huona si vya lazima.

Kwa mantiki hiyo, watu hao wanapaswa kuyaendeleza mazuri yote waliyokuwa wakiyafanya wakati wa Kwaresma kama kuacha kutumia vilevi, kufanya ibada na kuacha anasa. Kwa maneno mengine, yale mema waliyokuwa wakiyafanya ndani ya siku 40 za kipindi cha Kwaresma, wanapaswa kuyaendeleza hata ikibidi kufanya kwa viwango zaidi.


Tunasema hivyo kwa sababu imekuwa desturi ya baadhi ya watu kufanya mambo yanayompendeza Mungu na wengine hata kutubu lakini baada ya kumalizika kwa kipindi hicho, hurudi kufanya mambo mabaya na mengine chukizo kwa Mwenyezi Mungu na wanadamu.

Kwa mantiki hiyo, watu wamrudie Mungu na kutenda mambo mazuri ikiwamo kuwa na moyo wa huruma na upendo kwa wanadamu wenzao.

Aidha, kwa kuwa sikukuu hii na zile zinazovuta watu wengi husherehekewa kwa matukio mbalimbali, ni vyema vyombo vya ulinzi na usalama vikaimarisha ulinzi katika maeneo mbalimbali yakiwamo ya ibada na starehe.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Enzi za wagombea kupita bila kupingwa zimepitwa na wakati

Na Sabato Kasika

**LIMEKUWA** jambo la kawaida kusikia katika siasa wagombea wakipita bila kupingwa kila unapofanyika uchaguzi, uwe wa viongozi wa serikali za mitaa na vitongoji au wa rais, wabunge na madiwani.

Hatua hiyo imekuwa ikizua malalamiko kutoka wagombea ambao majina yao huenguliwa kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo za kutojaza taarifa zao vizuri katika fomu za kuomba kuteuliwa nafasi ya uongozi kwenye uchaguzi.

Mfano, katika uchaguzi wa viongozi wa serikali za mitaa na vitongoji wa mwaka 2019, ulizua malalamiko na kusababisha baadhi ya wagombea kuususia wakidai kuwapo 'figisu' za kuwabeba wagombea wa chama tawala.

Kwa mfano katika wilaya moja ya Kinondoni mkoani Dar es Salaam ilikuwa na mitaa 106 ambayo wagombea kutoka vyama mbalimbali walijitokeza kuwania nafasi ya mwenyekiti.

Hata hivyo, mitaa 105 wagombea wa CCM walipita bila kupingwa katika nafasi zote, ila mmoja tu. Hiyo ni taarifa iliyotolewa wakati huo na aliyekuwa msimamizi wa uchaguzi wa Manispaa ya Kinondoni mwalimu Kiduna Mageni.

Viongozi wakuu wa vyama vya upinzani walitangaza kususia uchaguzi huo, kutokana na kile walichodai kuwa kulikuwa na kila dalili za kuwabeba wagombea kutoka CCM na hivyo wakajiweka pembeni.

Mtindo huo haukuishia hapo bali hata katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, wagombea ubunge 28 wa CCM walipita bila kupingwa katika majimbo yao ingawa inaelezwa kuwa kulikuwa na wapinzani.

Lakini kama waswahili wasemavyo kwamba kila chenye mwanzo hakikosi mwisho, huenda ndivyo ikawa, kwani baada ya malalamiko ya muda mrefu kuhusu mtindo huo wa kupita bila kupingwa, umepigwa 'stop'.

Ninasema huenda ikawa mwisho, kwa sababu Mahakama Kuu ya Tanzania imebatilisha vifungu vya sheria vinavyoruhusu kuwapo kwa wabunge na madiwani wa aina hiyo.

Uamuzi wa mahakama hiyo ulifikiwa hivi karibuni, katika hukumu ya kesi ya kikatiba, iliyofunguliwa na mwana siasa, mwanachama wa chama cha ACT-Wazalendo, Joran Lwehabura Bashange, baada ya kukubaliana na hoja zake.

Alifungua kesi hiyo Mahakama Kuu Masjala Kuu, Dar es Salaam, dhidi ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, akipinga kuwapo wabunge na madiwani wanaotangazwa kupita bila kupingwa.

Katika kesi hiyo ya kikatiba namba 19 ya mwaka 2021, alikuwa akihoji uhalali wa kikatiba wa kifungu cha 44 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Sura 343 kinachoruhusu kuwapo kwa wabunge wanaopita bila kupingwa.

Pamoja na hayo, alikuwa akihoji pia uhalali wa kikatiba wa vifungu vya 45(5) na 13 (7) vya Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Sura 292 vinavyoruhusu kuwepo kwa madiwani wanaopita bila kupingwa.

Katika hukumu hiyo ambayo ilitolewa na jopo la majaji watatu waliosikiliza kesi hiyo; John Mgetta (kiongozi wa jopo), Dk. Benhajj Masoud na Edwin Kakolaki, mahakama ikasema vifungu hivyo vinakinzana na Katiba.

Mahakama ikasema ni batili kwa kukiuka masharti ya Ibara ya 21(1) (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kama ambavyo imekuwa ikirekebishwa mara kwa mara na kwamba wanaendelea kuvitupilia mbali vifungu hivyo kutoka katika vitabu vya sheria.

Ninadhani kwa uamuzi huo hakutakuwa na ushindi wa mezani ambao umekuwa ukizusha malalamiko kwa wanasiasa na wadau wa siasa hasa pale baadhi ya wagombea wanapoenguliwa ili mmoja apite bila kupingwa.

Ingependeza kama wapiga kura wakaachwa wachague wenyewe mgombea au mtu wanayemtaka awe kiongozi wao, badala ya kuwaachia mgombea mmoja ambaye huenda ni chaguo lao au si chaguo lao.Kuendelea kuwapo kwa wagombea wanaopita bila kupingwa ni sawa na kuwapa ushindi wa mezani ambao wanaupata kirahisi bila kuhangaika, mwisho wa siku hawawezi kuwatumikia wananchi.

Ninaamini uamuzi wa kuondoa mtindo wa wagombea kupita bila kupingwa utasaidia kuwafanya wanasiasa kupimana ubavu kwa hoja, ili mwisho wa siku wanaopigakura ndio waamue ni nani anafaa kuwa kiongozi wao.

## FIKRA MBADALA

# Heri ya sikukuu ya Pasaka Wakristo, swaumu njema wenzetu waislamu



Pascal Mayalla

KWA vile Jumapili ya leo imedondokea sikukuu ya Pasaka, safu yangu itajikita kwenye kusherehekea siku hii kwa kuwatakia Wakristo Pasaka njema. Lakini kwa vile pia imedondokea wakati wa mwezi Mtukufu wa Ramadhan, pia nawatakia ndugu zetu Waislamu mfungo mwema.

Kuna msemo wa kizungu usemao “charity begins at home” na “the greatest love of all is learning to love yourself”. Misemo hii ina maana kwamba mtu ukiwa mwema, wema huo uanzie nyumbani kwako na mapenzi makubwa kuliko mapenzi yoyote ni kujifunza kujipenda kwanza ndipo uwapende wengine. Kwa hiyo nawaomba mnisamehe kwa makala ya leo kuanza kwa kujipenda na kujipendelea.

Huyu Paskali anayeandika makala hii, tarehe kama ya leo, zaidi ya miaka 50 iliyopita, Aprili 8 enzi za miaka ya 1960 alizaliwa na ikatokea kitu kinachoitwa ‘coincidence’ Aprili 8, mwaka jana, kilizaliwa kitoto kitindamimba changu ki Paskali Kidogo (Pasco Jnr) ambacho wanakiita kwa kifupi ki PiiJei (PJ). Hivyo jana Jumamosi usiku baba na mtoto walisherehekea siku yao ya kuzaliwa kwa kuhudhuria Ibada ya Pasaka katika Kanisa Katoliki Parokia ya Bikira Maria Mama wa Huruma, Mbezi Beach mkoani Dar es Salaam.

Kwa sisi Wakristo, ukimsikia mtu yeyote anaitwa Pasco, Paskali, Paskalia, Paskalina, Paskazia au Ester, ujue alizaliwa siku ya Pasaka hivyo nawatakia heri siku ya kuzaliwa wote walizaliwa Pasaka.

Sikukuu ya Pasaka huwa haina shamrashamra sana za maandalizi ya kusherehekea kama Krismasi kwa sababu imetanguliwa na mfungo wa Kwaresma. Sijui ni kwa nini hali huwa iko hivi labda kutokana na mateso na kifo msalabani ile Ijumaa Kuu, hivyo ufufuko si wa shamrashamra.

Katika funga yetu Wakristo, kutokana na kufunga kwa siri, sijawahi kusikia kufuturu popote, lakini mfungo wa wenzetu Waislamu, mwezi Mtukufu wa Ramadhani, kila uchwao utasikia watu, taasisi hadi serikali wakifuturisha. Sikukuu ya Pasaka hata zisiponunuliwa nguo mpya kwa watoto, nyumbani panakalika lakini kwa Krismasi kusiponunuliwa nguo mpya kwa watoto hapakaliki!.

Sikukuu ya Pasaka inapooza kutokana na kutanguliwa na mfungo wa Kwaresma lakini mbona sikukuu ya Iddi El Fitri inatanguliwa na mfungo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhan lakini ina shamrashamra za kutosha?. Tena Iddi kwa wenzetu Waislamu ni lazima watoto wapate nguo mpya na hata sisi Wakristo wa Uswahilini uswazi, ili kuwaepushia watoto wetu kuwa wanyonge, unaweza usiwanunulie nguo mpya Pasaka, lakini Iddi... thubutu!, lazima utanunua!.

Sikukuu ya Pasaka Kikristo inasherehekewa kwa Fumbo la Pasaka. hili fumbo la Pasaka ndio msingi wa imani ya Ukristo Fumbo la Imani Kristo Alikufa, Kristo Alifufuka, Kristo Atakuja tena!.Fumbo hili ni kuadhimisha ufufuko wa Bwana wetu Yesu Kristo kwa kasulubiwa pia kwa ajili yetu; akateswa kwa mamlaka ya Pontio Pilato, akafa, akazikwa, akafufuka siku ya tatu kama ilivyoandikwa katika maandiko matakatifu.

Fumbo la Pasaka ni kiini cha imani ya kanisa inayopaswa kutangazwa na kushuhudiwa kwa watu wa mataifa. Kwa njia ya mateso, kifo, ufufuko kutoka kwa wafu na kupaa mbinguni, mwanadamu amekombolewa kutoka katika wafu.

Kuteswa kwake kwa kupigwa mijeledi, kuvikwa taji la miiba, kutemewa mate, kutundikwa juu ya msalaba, kufa na kuzikwa. Hivyo ufufuko wake ni hitimisho la yote haya ambayo tunayaona kuwa ni ya kawaida. Ufufuko ndio hasa kilele cha fumbo la ukombozi wa ukristo.

Ufufuko wa Bwana wetu Yesu Kristo ni hakika. Wakristo hatupaswi kutilia shaka. Tunazo kila sababu za kuamini na kuushuhudia. Kwanza kaburi li wazi na mwili wake haupo na ni wazi haukuibwa maana kaburi lililindwa na askari na vitambaa alivyozungushiwa vipo vimezongwazongwa pembeni. Malaika wanashuhudia hili na Yesu mwenyewe alionekana kwa wafuasi wake, akajifunua kwao katika neno lake nao walimtambua katika kuumega mkate.

Wanawake waliokwenda alfajiri kaburini kuupaka mwili wake mafuta nao wanashuhudia kuwa amefufuka naye amewatokea. Baada ya kufa Yesu kristo, wafuasi wake walijawa na woga mwingi hata wakajifungia ndani kwa hofu ya Wayahudi. Kilichowapa nguvu ya kutoka kwa ujasiri na kutoa ushuhuda mbele za watu bila woga ni ufufuko. Hili linajidhihirisha wazi katika hotuba ya Petro akitoa ushuhuda wa ufufuko wa Yesu kwa ushujaa na ujasiri wa ajabu tena mbele yao waandishi na mafarisayo. Kama Yesu asingefufuka wanafunzi wake wangetawanyika na kanisa lisingezaliwa na kudumu kama ilivyotokea. Hivyo nasi tuwe na ujasiri wa kuishuhudia imani yetu bila woga wala mashaka.

Ufufuko wa Kristo ni wokovu wetu. Hakika tumekombolewa kutoka mautini na tumewekwa huru kutoka utumwa wa shetani na upotevu wa milele. Mlango wa paradiso uliofungwa kutokana na dhambi ya asili ya Adamu wa kwanza, umefunguliwa kwa kifo na ufufuko wa Adamu wa pili, yaani Yesu Kristo. Pasaka kwetu ni siku ya kurejesha matumaini baada ya kuwa tumekata tamaa ya maisha kutokana na magonjwa ya mwili na roho, hali ambayo ilisababisha kujiona tumeshindikana kwa tabia zetu chafu, kujiona hatufai katika jumuiya.

Pasaka ni Habari Njema kwetu kwamba Kristo Mfufuka yuko kati yetu, yupo pamoja nasi na ndani ya kila mmoja wetu. Ameshinda dhambi na kifo, nasi pia tutashirikishwa ushindi huu endapo tutamruhusu akae nasi na kama tutatelekeza yale aliyoamuru. Mkristo usikie kama bado hujaachana na chachu ya uovu na ubaya.

Kwa tendo hilo umoja wetu na Kristo mfufuka unaimarishwa kwani katika ubatizo tulikufa na kufufuka na Kristu; tukaahidi kumfuata daima katika maisha ya taabu na raha. Yatupasa kuishi kadiri ya ahadi zetu za ubatizo.

Mtihani mkubwa na changamoto kubwa kwetu sisi Wakristo baada ya mfungo wa Kwaresma na Waislamu baada ya mfungo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani, tunapaswa kuendelea kuishi kwa kutenda mema na sio kuyarejelea yale maovu tuliyoyaacha tulipofunga!.

**Pasaka Njema**
**Paskali 0754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Asiyefanya kazi na asile ifanye kazi!



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

MIONGONI mwa semi maarufu katika jamii na zinazopatikana hata kwenye Biblia Takatifu ni ule wa ‘Asiyefanya kazi na asile!’ Ukimaanisha kuwa bila kazi hakuna uzalishaji na hivyo hakuna chakula.

Maana halisi ya usemi huu, si kwamba asiyefanya kazi basi anyimwe kula, la hasha, ni kwamba bila chakula hakuna cha kula. Kwa maana nyingine, asiyefanya kazi si lazima anyimwe kula.

Hiyo inathibitishwa na kuwapo kwa wenye ulemavu katika jamii, kwamba ulemavu wao si kigezo cha kutokula, kwa kuwa tu hawafanyi kazi. Lengo la usemi huo ni kuwa kama una nguvu ya kuzalisha, zalisha.

Kwamba usiwe na nguvu ukaacha kuzitumia kuzalisha chakula ili ule wewe na wengine wasio na nguvu hizo, kwa sababu moja au nyingine. Lakini wakati mwingine usemi huu ulitumika visivyo.

Tunakumbuka utawala uliopita wa ‘Hapa Kazi Tu’, ulivyokuwa unautumia usemi huu kukataza watu kula kwa sababu tu hawakufanya kazi! Hii haikuwa sawa kwa sababu kutofanya kazi kulitegemea mazingira na muktadha katika jamii.

Kama kigezo cha kutofanya kazi ndicho kilitumika kunyima watu kula, basi kikitumika leo wengi watakufa njaa, kwa kuwa hawafanyi kazi ama kwa kukosa kazi au hali halisi ya mabadiliko ya tabianchi. Si siri, kuwa nchini hivi sasa ajira ni tatizo, kwani wenye sifa za kupata ajira ni wengi lakini nafasi hakuna, kwa sababu hatuzalishi vyanzo vingi vya kazi, na matokeo yake, tunahubiriana kujiajiri ambako ni kizungumkuti.

Tunasomesha watu wengi, lakini wanahitimu na kurudi mitaani kuzurura, kutafuta ajira, huku wenye ajira wakiwataka wasio na ajira kujiajiri kwa mikopo ambayo inatolewa kwa kutazamana sura.

Watanzania tunashuhudia mabadiliko ya tabia nchi yanavyotuathiri, mpaka wakati mwingine kukosa umeme na maji. Tumekuwa tukiingia kwenye mgawo wa maji na umeme, tukashusha uzalishaji viwandani kwa mgawo wa nishati hiyo, kuna nyakati viwanda vikasimama kuzalisha.

Tumeelekeza mawazo na fikra zetu kwenye bwawa la Mwalimu Nyerere linaloendelea kujengwa kwa matarajio ya kupata umeme utakaokidhi mahitaji na hata kusaza, na kuuza nje ya nchi na kusahau gesi asili tuliyoigundua Mtwara.

Gesi ilipopatikana, tulishangilia na mawazo yetu kuhamia huko kwa matarajio makubwa ya kumaliza tatizo la umeme, lakini pia matumizi ya kuni na mkaa na kuokoa mazingira na kuepukana na janga la nchi kuwa jangwa.

Kukiwa na mgawo sehemu, bila shaka mitambo haifanyi kazi na hivyo kuhitaji rasilimali watu, maana yake ni kwamba hakuna anayefanya kazi wakati huo, je asiyefanya kazi na asile ikitumika, wafanyakazi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) watasalimika?

Hali kadhalika, wakati hakuna maji eneo lenye mgawo, ina maana mitambo imesimama kama si kupunguza uzalishaji na hivyo kutokuwapo umuhimu wa raslimali watu, je wafanyakazi wa mamlaka za majisafi watasalimika kufa njaa?

Ni dhahiri kuwa kwa mujibu wa mikataba, wafanyakazi wanaendelea kuwa sehemu zao za kazi hata kama hakuna huduma kwa asilimia 100. Hivyo, hata kama hawatafanya kazi lazima watakula tu.

Matokeo yake ni kwamba kwa kuwa na uhakika wa kutoguswa na usemi wa ‘Asiyefanya kazi na asile’, hawataona umuhimu wa kutafuta suluhisho la kudumu la matatizo yanayokumba wananchi wanaowategemea kwa huduma zao.

Na hii ndiyo sababu kuu ya kwa nini nchi katika miaka yake 61 ya uhuru, bado inasuasua na matatizo ya maji na umeme, kutokana na wahusika kutoguswa na matatizo hayo, kwa sababu tu kwao asiyefanya kazi anakula. Atalipwa mshahara na posho na mambo mengine, hata kama hakuna maji wala umeme.

Hivyo sasa Watanzania tunahitaji viongozi na wafanyakazi wabunifu katika sehemu zao za kazi na maeneo yao ya uongozi, badala ya kuwa na wanyapara watoa amri, bila kutoa uongozi wa nini kifanyike kutatua matatizo kwa muda wote.

Rais Samia Suluhu Hassan alipata kusema kweli, kwamba kuna watu wanaishi kwa kumwangalia yeye kwa kila kitu, wakiogopa kuamua wakidhani wataharibu, bila kutambua kiongozi mkuu wao anachokitaka ni nini, na hii husababisha maendeleo kukwama.

Imekuwa hivyo, kwani ni dhahiri viongozi hao wanasubiri kutatua matatizo ya wananchi mpaka wanaposikia au kumwona Rais amefika maeneo yao, ndipo hujifaragua kuyazungumzia huku mengine akiyashuhudia kwenye mabango.

Anachokifanya Rais Samia ndicho kinachotakiwa na Watanzania, kwamba miaka mingi maneno yamekuwa yakitawala majukwaa ya kisiasa huku wananchi wakiendelea kuumia, kazi yao ikiwa ni kupiga kura na kutelekezwa baada ya ushindi.

**Alamsiki! Heri ya Pasaka!**

## DC atengua uamuzi M/kiti kuondolewa

**Na Steven William,** NACHINGWEA

MKUU wa wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi, Mohamed Moyo, ametengua uamuzi wa wajumbe wa Serikali ya Kijiji cha Naipingo, wa kumwondoa madarakani Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji, Christopher Ngunyali, kwa madai ana tuhuma mbalimbali.

Wajumbe hao walimwondoa madarakani mwenyekiti huyo na kuandika barua ofisi ya Mkuu wa Wilaya kuhusu tuhuma zinazomkabili.

Kutokana na sakata hilo, Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, Mohamed Moyo, Alhamisi alifika kijijini hapo baada ya kupokea malalamiko yaliyowasilishwa na mtendaji wa kata ya Naipingo.

Moyo alipofika katika mkutano kijijini hapo, alitengua uamuzi huo kwamba ni batili na kusisitiza kuwa utaratibu ulikiukwa ikiwamo kutokuwapo kwa vikao halali vya kumwondoa kiongozi huyo aliyechaguliwa na wananchi.

Alisema serikali ya kijiji hicho ina wajumbe 25 ambao wanaweza kutoa uamuzi wowote wa serikali ya kijiji lakini katika kujadili suala la mwenyekiti, walikuwapo wajumbe 11.

Moyo alisema hapingi malalamiko hayo bali anachopinga ni namna ambavyo utaratibu ulitumika kumwondoa mwenyekiti kwenye nafasi ya uongozi.

Alisema kutokana na ukiukwaji huo, amemrejesha kwenye nafasi ya uongozi kwa kuwa kikao kilichofanywa hakikuwa kikao halali kwa kuwa mwenyekiti wa kikao hicho hakuwa miongoni mwa wajumbe ili kufanya uamuzi.

Kwa mujibu wa Moyo, wajumbe wanatakiwa kurudi kwenye vikao halali ili kumwondoa mwenyekiti huyo kama wanataka kwa kufuata utaratibu unaotakiwa kama vile wajumbe kufikia robo tatu ya akidi na kupiga kura au chama kiamue kumfuta uanachama.

Moyo alisema Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Naipingo, hakina mamlaka ya moja kwa moja kumwondoa madarakani mwenyekiti huyo bali mwenye mamlaka ni mkuu wa wilaya kwa kufuata sheria na kanuni za nchi.

Katibu wa CCM Kata ya Naipingo, Angelus Chinguile, alisema chama kilifuata taratibu zote zinazotakiwa lakini tatizo lipo kwa uongozi wa serikali ya kata.

Mwenyekiti anayetuhumiwa, alisema kuna baadhi ya wajumbe wa serikali ya kijiji wanamchukia kwa utendaji wake kazi wa kusimamia sheria.

# Jafo akerwa viwango duni vya lambo

**Na Mwandishi Wetu,** MPWAPWA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, ameagiza kufanyika kwa marekebisho katika lambo lililochimbwa katika Kijiji cha Kazania, Mpwapwa mkoani Dodoma ili lizalishe maji kwa kiwango kikubwa kama ilivyotarajiwa.

Jafo alitoa agizo hilo juzi alipofanya ziara ya kushtukiza katika kijiji hicho kukagua lambo hilo lililochimbwa kupitia Mradi wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi kwa Kutumia Mfumo Ikolojia Vijijini (EBARR) unaoratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais.

Lambo hilo halijajaa maji inavyotakiwa pamoja na kunyesha kwa mvua katika siku kadhaa zilizopita, akirejea ziara aliyofanya Desemba 22, mwaka jana alionyesha wasiwasi wa namna lambo hilo lilivyokuwa likichimbwa.

Wakati wa ziara hiyo, alionyesha wasiwasi huenda lisijae maji akisema japo si mtaalamu alitoa ushauri kwa wataalamu wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ambao ndio wanafanya usanifu wa malambo kuzingatia kujenga mifereji ili kujaza maji kwa haraka.

"Ofisi ya Makamu wa Rais imetoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hii ya mazingira na tume ndiyo inaelekeza maeneo sahihi ambayo uchimbaji wa malambo unaweza kufanyika. Lakini hapa tume mmetuangusha, nilitegemea katika mvua hizi lingekuwa limejaa na hapa naona wananchi wanachota maji yenye rangi hii ya udongo na yangekuwa meupe kama yangekuwa yamejaa kwenye lambo," alisema.

Kutokana na hali hiyo, aliwaagiza wataalamu wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kufanya marekebisho ya lambo ikiwamo kutengeneza mifereji ifikapo Juni, mwaka huu ili maji yapite kwa urahisi tofauti na ilivyo sasa.

Waziri Jafo alisema maeneo mengi ya Dodoma yanakabiliwa na ukame kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi, hivyo wananchi hawana budi kuendelea kupanda miti kwa wingi ili kukabiliana na hali hiyo.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Mpwapwa, Sarah Komba, aliishukuru serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kutekeleza mradi huo wilayani hapa na kusema wananchi wameupokea vizuri.

Alisema lambo hilo limejengwa kimkakati na kuahidi litatunzwa na kutumika vizuri kama inavyotarajiwa ili liweze kuwanufaisha wananchi na kuondokana na adha ya uhaba wa maji unaowakabili.

Diwani wa Nghambi, Richard Milimo, alitoa wito kwa wataalamu kuzingatia ushauri aliotoa Waziri Jafo kuhusu kujenga mifereji ili kuongeza ujazo wa maji kuingia katika lambo hilo.

Mratibu wa Mradi wa EBARR katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, Aziz Bilu, alisema uhaba wa mvua umechangia pia kutojaa kwa lambo hilo kwa wakati ambapo imenyesha kwa siku saba katika miezi minne.




Mwakilishi wa Kampuni ya REMGRO, Salvatory Shirima (kushoto), akikabidhi msaada wa vyakula kwa mlezi wa Kituo cha watu wenye mahitaji maalum cha Msongola, Christina Haule, kwa ajili ya Sikukuu ya Pasaka, Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Othman asisitiza malezi kwa ustawi

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amehimiza jamii kuendelea na malezi mema ili kupata vijana wenye maadili mema wanaoweza kuitumikia jamii na kusaidia kasi ya upatikanaji wa maendeleo.

Othman aliyasema hayo katika kijiji cha Masipa Pandani wilaya ya Wete, Kaskazini Pemba alipotoa salamu kwa wakazi wa kijiji hicho baada ya kushiriki futari ya pamoja aliyoandaliwa.

Alisema hivi sasa jamii imekumbwa na janga la ukosefu wa maadili katika vyombo mbalimbali vikiwamo mahakama na mamlaka zingine, hivyo kuchangia watu kukosa haki zao. Alisema hiyo inatokana na watendaji wengi kukosa maadili.

Othman aliitaka jamii na wazazi kuendelea na malezi mema kwa vijana ili kuzalisha watu wenye heshima na maadili wanaoweza kuaminiwa kwa kutumikia watu ndani na nje ya taifa kwa uadilifu mkubwa utakaoiletea nchi heshima.

Alihimiza ushirikiano katika jamii sambamba na kuendelea kufungamana na mafunzo ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ili kupata fadhila za mwezi huo.

Pia alisema kuishi katika mafunzo ya maadili na nidhamu kubwa inayopatikana katika mwezi mtukufu wa Ramadhani, kutalifanya taifa kuendelea kuwa na mshikamano, amani na ushirikiano wa kweli katika kuliletea taifa maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Othman alikuwa kisiwani Pemba kwa ziara ya siku nne ambayo pamoja na kutembelea wagonjwa katika wilaya zote za Pemba pia alifanya futari ya pamoja iliyowashirikisha wananchi, viongozi wa siasa na serikali katika mikoa ya Kaskazini na Kusini Pemba.

Ziara kama hiyo aliifanya katika mikoa ya Unguja na kupata nafasi ya kuwajulia hali wagonjwa wa mikoa mitatu ya Mjini Magharibi, kusini Unguja na Kaskazini Unguja.

# MAISHA

APRILI 9, 2023

Nipashe

Baba, Mama na Mwana


Jumapili




Ukurasa 14


## Bachela furahia pilau la sikukuu

## MAISHA NI NYUMBA



Ukurasa 15

Kitanda cha chuma nyumbani na faida zake





## KATUNIKA


Ukurasa 16



# USO UNAOTABASAMU

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA




| | | | |
|---|---|---|---|
| 3 | 4 | 1 | 2 |
| 1 | 2 | 4 | 3 |
| 4 | 3 | 2 | 1 |
| 2 | 1 | 3 | 4 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| C | H | A | ■ | M | B | A |
| H | ■ | ■ | ■ | S | ■ | S |
| U | ■ | P | A | O | ■ | H |
| T | U | A | ■ | M | T | I |
| A | ■ | M | E | I | ■ | K |
| M | ■ | B | ■ | ■ | ■ | W |
| A | N | A | ■ | M | K | E |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

ADA, PEA, LOA, ANA, NOA, GIA, NIA, IPO, GONGA, PEANA, ANGAZWA, LIPIZIA

## TOA TOFAUTI 5




## AMSHA AKILI




## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

MTOTO John alikuwa akitembea na mama yake, mara alimuona mtu akimnyoa nywele mwenzake wakiwa chini ya mti. Alipoona watu hao John alianza kulia huku akizishika nywele zake.

Mama: John unalia nini mwanangu, mbona tulikuwa tunatembea vizuri?

John: Mama si umemuona yule mtu akimnyoa nywele mwenzake naogopa sana

Mama: Kwa nini?

John: Mwalimu alisema ukiona mwenzako ananyolewa, wewe tia maji kichwani

Mama: We John huo ni msemo tu, unamaanisha kile kinachompata mwenzako kinaweza kukupata na wewe, hivyo usimcheke.

John: Kumbe

**SWALI**

Zao la Kakao linalimwa wapi nchini Tanzania?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Kwa nini wanandoa waachane na kuanzisha nyumba nyingine?

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na vimbwanga vya Maisha Ndivyo Yalivyo. Yuko msomaji wetu mzuri alinitumia ujumbe kwenye mtandao wa WhatsApp, akielezea aliyopitia ili kuwa kielelezo kuwasaidia wengine.

Alikuwa akijaribu kuonyesha ni kwa nini mwanaume aihame nyumba yake na kuanzisha nyumba nyingine?

Alijieleza vyema nikaona ni vema nikumegee na wewe msomaji wangu tuweze kujadili pamoja. Hili ni tatizo kubwa sana katika jamii yetu. Ni hoja nzito na inahusu jambo ambalo limezikumba familia nyingi zisijue chanzo chake.

Katika maelezo yake akasema hivi;-Nikiwa katika ajira ya taasisi mojawapo ya kisheria, nimekutana na matatizo mengi sana ya kuvunjika ndoa ambapo mmoja wa wanandoa huondoka na kuanzisha nyumba mpya.

Uzoefu wangu umenionyesha kuwa asilimia kubwa ya wanaume wanaokimbia wake zao na kuanzisha ndoa nyingine wanasukumwa na mambo mawili makubwa.

Kwanza ni kupanda kwa hali ya mapato ya familia. Wanandoa wanaoana wakiwa duni. Katika hali hiyo umaarufu wa mume au mke unakua ni mdogo sana. Jinsi mapato yanavyoongezeka ndivyo na heshima na umaarufu wao unavyozidi kukua.

Hapo marafiki wanaongezeka, kama mume alikua hasafiri nje ya kijiji au mji wake, sasa ataanza kusafiri.Kama alikua ni karani na sasa amesoma na kuwa ofisa, ataanza kuhudhuria semina, vikao na outings za kikazi kibao.

Hivyo atabadilika kimavazi, ustaarabu, upeo wa ufahamu na kadhalika.Endapo mwenzi wake wa ndoa hataendana na mabadiliko hayo, haraka mume huyo ataanza kuona kupwaya kwa mwenza wake.

Huko nje atakutana na wamama wanaojua kuvaa, kuongea kukaribisha na hata kutunza nyumba. Haraka atajiona mnyoge mbele ya wengine.Wazo la kupata mbadala wa kuziba pengo hilo huanza.

Taratibu mume huyo huanzisha uhusiana usio rasmi pembeni na mwisho uhusiano huo humteka na kuhamia huko kabisa. Lakini kiini ni mabadiliko ya kiuchumi, kutokuwa na elimu au mapato mengine.

Angalizo kwa wenzi wa ndoa hapa ni kujitahidi kwenda sambamba na mabadiliko hayo pasipo mmoja kuachwa nyuma. Hiyo ni moja ya siri kubwa katika mahusiano na pia maisha ya ndoa.

Sababu ya pili ni kutokuwa makini tokea awali wakati wa kufanya chaguo la mwenzi wa ndoa. Hapa inawezekana sababu ni uchumba kuwa wa muda mfupi baada ya wawili hao kujuana, au ndoa za utotoni.

Na kwa mantiki hiyo, baada ya muda mfupi wa maisha mume anagundua kuwa huyo si saizi yake au hakuwa chaguo lake. Hali inakuja ile ile anaanzisha uhusiano usio rasmi na yule ambaye anadhani anafiti zaidi.

Uhusiana ukinoga anahama mzima mzima. Angalizo kwa maeneo ya vijijini ndoa za utotoni ni tatizo kubwa sana. Kijana anaozwa binti mdogo kwa sababu wazazi wana uwezo wa kulipa mahari. Wanapopevuka wote wanajigundua huyo aliye naye hakuwa chaguo. Katika hali hii mara nyingi mke ndiye hukimbiwa. Msomaji Singida.

Msomaji wangu, bila shaka umemsikia vema msomaji wetu huyo. Nami ninayo machache ya kuongezea kuhusu mmoja wa wanandoa kuhama mji wake na kutengeneza maisha kwingine.

Roho ya ubabe inaweza pia kumfanya mmoja wa wanandoa. Wakati wawili wakisaka mwenza wa kuishi naye, huwa wapole, wanyenyekevu, wasikivu, waliojaa upendo kwa kuwatizama kwa sura ya nje.

Lakini kumbe vyote hivyo havimo ndani ya mioyo yao. Kumbe ndani kumejaa jeuri, ukatili, uhuni wa kila aina, ulevi wa pombe na uvutaji wa sigara na kadhalika. Vyote hivi havionekani kwa nje. Hujifunua baadaye baada ya ndoa kutulia.

Hizi ni tabia zilizojificha ambazo zitakapojitokeza hadharani, ndipo mitafaruku huibuka na kuonekana ni jambo jipya kumbe lilikuwepo.

Eneo lingine ni kuzidiana kipato. Wapo wanaooana wakiwa wote wana uchumi mzuri. Wengine mmoja mfano baba ana uwezo mkubwa kiuchumi kuliko mama. Wengine mama ana uwezo mkubwa kuliko baba.

Baba ni kiongozi wa familia. Inapotokea kipato chake ni kidogo na mke anamzidi, wakati mwingine hujisikia vibaya. Mwanamke huyu huweza kumdharau mumewe na manyanyaso yakizidi, mume hutafuta mchepuko kutuliza akili. Wapo walioenda wakarudi, wengine walizamia huko huko na kuanzisha miji mipya, maisha yaendelee.

**Bila shaka umejifunza jambo hapo. Je, una kisa? Ujumbe 071 5268581.**

## WARAKA WA NDANI



Na Godfrey Mushi

# Mfugaji usiogope ng'ombe wako kukurushia teke

MFUGAJI aliyejaliwa hekima na uvumilivu katika muda wote wa uongozi wake, hata nje ya madaraka yake, hawezi kumlaumu ng'ombe ambaye amekuwa akimchunga, kumkatia majani, kumpa maji na kumlisha pumba nyakati za ukame.

Ng'ombe wengi hata ukiwafanyia nini, bado ng'ombe huyo huyo unayemtumikia anaweza kukupiga teke na hata kukuumiza. Iko mifano mingi ambayo imejitokeza kwamba ng'ombe kuumiza anayemlisha.

Yamkini ng'ombe unayemsumbukia, siye anayezalisha wala kuongeza uzao, ila inaweza kuwa ni ishara kwako kwamba jitoe bila kusubiri fadhila, kwa sababu kati ya ng'ombe mmoja kisirani, wako wawili watakaokupa maziwa.

Nimelazimika kuanza na mfano huo ili kuwatia moyo Rais Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa kwa namna wanavyopambana kuijenga nchi, kuweka mazingira bora na wezeshi kwa makundi ya jamii kufikia maendeleo yao kiuchumi na taifa kwa ujumla wake. Lakini wako wachache wanaojaribu kuharibu mazuri wanayoyafanya, na wengine kukejeli kazi zinazofanyika kila kona ya nchi.

Aprili 5, mwaka huu, Waziri Mkuu Majaliwa, wakati anawasilisha hotuba yake Bungeni, kuhusu mapitio na mwelekeo wa kazi za serikali na makadirio ya mapato na matumizi ya fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge, kwa mwaka 2023/24, alisema miradi 119 ya maendeleo yenye thamani ya Sh. bilioni 46.04 inachunguzwa, baada ya kubainika kuwa na kasoro mbalimbali katika utekelezaji wake.

Nilifarijika sana pale nilipomsikia akisisitiza kwa sura ya kazi kwamba serikali itaendeleza mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi, kwa kuweka kipaumbele katika kuzuia vitendo vya rushwa.

Kuhusu reli ya SGR, Waziri Mkuu alinukuliwa akisema mwaka 2022/23, serikali imefanya ununuzi wa vifaa vya uendeshaji wa reli ya SGR, ambapo utengenezaji wa mabehewa 59 ya abiria umefikia asilimia 92 na kwamba kati ya mabehewa hayo, 14 yaliwasili nchini Novemba, 2022 na 45 yaliyobaki yanatarajiwa kuwasili Mei, mwaka huu.

Aidha, alinukuliwa akisema utengenezaji wa vichwa vya treni 17 vya umeme na seti 10 za treni kwa ajili ya treni ya abiria umefikia asilimia 31.6 na seti moja ya treni hizo inatarajiwa kuwasili Juni, mwaka huu. Halafu pia utengenezaji wa mabehewa 1,430 ya mizigo umefikia asilimia 35.

Kwa juhudi hizo za serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan, naamini upatikanaji wa vifaa hivyo, utaboresha na kuongeza kiwango cha ubebaji mizigo na kupunguza gharama za usafiri na usafirishaji na hivyo kupunguza gharama za maisha.

Kazi nyingine ya kupongezwa serikali hii ni suala la hifadhi ya jamii, kwamba sekta ya hifadhi ya jamii imekuwa na mchango mkubwa kwenye uchumi pamoja na ustawi kwa wananchi. Kwenye hili kama Watanzania, tusifikirie kutupa mateke ili kuumiza mtu, viongozi wetu wakuu na serikali yake sikivu inastahili pongezi, hata kama hutaki, kweli itabaki kuwa kweli!

Hata utashi wa Rais Samia wa kuamua kulipa stahiki za Watanzania, hamuoni anastahili kufarijiwa? Kumbukumbu zilizoingia kwenye Hansard (kumbukumbu rasmi za Bunge), zinaonyesha hadi kufikia Februari, mwaka huu, deni la Sh. trilioni 2.17 limelipwa katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF).

Katika mwaka 2022/23, PSSSF imelipa mafao kwa wastaafu, wategemezi na wanufaika wengine 41,939, Sh. trilioni 1.074 na pensheni ya kila mwezi ya Sh. bilioni 507.28, sawa na wastani wa Sh. bilioni 63.41 kila mwezi kwa wastaafu 158,351. Hilo hamlioni? hebu tuache unafiki, pa kupongeza, pongeza!

Haya angalia, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), umelipa mafao ya Sh. bilioni 438.32 kwa wastaafu, wategemezi na wanufaika wengine wapatao 66,628. Kati ya kiasi hicho, Sh. bilioni 72.3 zililipwa kama pensheni ya kila mwezi kwa wastaafu 27,570 ni wastani wa Sh. bilioni 9.04 kwa kila mwezi.

Godfrey Mushi ni Mwandishi Mwandamizi wa Gazeti la Nipashe, Kanda ya Kaskazini.

***Anapatikana kwa barua pepe: ghandsome79@gmail.com.***

***Simu ya mkononi: +255 767 535490***





Magauni ya harusi yenye rangi ya bluu ni moja ya vazi linalopendekezwa kuvaliwa kwenye harusi. Pichani ni baadhi ya mitindo ya magauni yanayopendeza kuvaliwa na bi harusi.



# MITINDO



# KUWA KAMA ULIVYO

FULANA za polo ni vazi la kisasa zaidi na zinapendwa kuvaliwa na mastaa mbalimbali duniani.

Vazi hili linavaliwa na watu wa rika na jinsia tofauti wanapenda kuvaa nguo za kisasa katika shughuli zao mbalimbali.

Kwa mujibu wa wataalamu wa masula ya mitindo, wanasema nguo hizi hazina historia za nchi za kiafrika, lakini zimekuwa pendwa hasa kwa vijana.

Hapa nchini nguo za aina hii zimekuwa chaguo la kwanza kwa vijana na kuwafanya wabunifu na maduka ya nguo wanashindana kubuni mitindo mipya.

Fulana za Polo kwa kawaida imetengenezwa kwa kitambaa kigumu chenye mchanganyiko wa pamba na polista, na unapoiangalia utaona ina umbo jembamba.

Mara nyingi fulana hizi zinatengenezwa na kola pana eneo la shingoni, mikono yake mifupi kiasi na inayoshika ngozi. Urefu wake unaishia kwenye eneo la mkanda.

Kutokana na muonekano wake wa kuvutia, watu wengi hasa wanamichezo na watu maarufu wanapenda kuvaa wakiwa katika shughuli zao mbalimbali.

Fulana ya aina hii inapendeza sana kama mtu akifanya chaguo zuri la rangi.

Wataalamu wa mavazi wanashauri rangi nzuri ni ya samawati, machungwa, njano, bluu na bluu mpauko.

Unaweza kuvaa na suruali ya kitambaa, jeans au kaptura ya aina yoyote ile na ukatoka bomba.



URÉMBO

Na Mary Geofrey

# USO UNAOTABASAMU

KWA kutumia vitu vichache kutoka jikoni, unaweza kutengeneza na kupata 'kisugua ' uso bila kuwa na wasiwasi wa kupata madhara.

Kutumia kitu ulichotengeneza mwenyewe unaepuka kuingiza kemikali katika ngozi yako.

Tutakupa njia tatu na rahisi za kutengeneza kisugua usoni 'facial scrub' kutoka nyumbani kwa kutumia vitu vitatu.

Safisha kuondoa make-up, kusafisha mafuta, kukaza ngozi ya uso na kuondoa ngozi zilizo kufa.

Moisturizing huipa ngozi unyevu, kusafisha na kuondoa ngozi zilizo kufa.

**Namna ya kufanya**

Kusafisha ina kusaidia kuondoa makeup, kutoa mafuta na kuondoa ngozi zilizo kufa hapa ina saidia kukinga ngozi yako dhidi ya chunusi (vipele) na kufungua vishimo vilivyo zibwa, una hitaji vitu vitatu ambavyo ni ngano nzima, asali na mtindi.

Chukua kijiko kimoja cha hivyo vitu vitatu vyote ngano nzima, asali na mtindi.

Changanya hivyo vyote katika bakuli na anza kupaka kwa mtindo wa duara kuanzia kwenye kidevu mpaka kwenye komwe, kaa nayo kwa muda wa dakika mbili kisha futa kwa maji ya uvugu vugu ukimaliza osha tena kwa maji ya baridi ili kufunga vitobo na futa kwa taulo safi.

**Unyevushaji (Moisturizing)**

Ili kuipa ngozi yako unyevu na isiwe kavu sana una takiwa kuwa na vitu vitatu, limao, baking soda na asali.

Changanya kijiko kimoja cha sali, limao na baking soda anza kupaka kwa mtindo wa duara kuanzia kwenye kidevu mpaka kwenye komwe kaa nayo kwa muda wa dakika mbili kisha futa kwa maji ya uvugu vugu na futa kwa taulo safi.

Chukua kijiko kimoja cha asali, olive oil na sukari ya brown changanya anza kupaka kwa mtindo wa duara kuanzia kwenye kidevu mpaka kwenye komwe, kaa nayo kwa muda wa dakika mbili kisha futa kwa maji ya uvugu vugu na futa kwa taulo safi.







MAPISHI

Na Mary Geofrey



# Bachela furahia pilau la sikukuu

KAMA wewe ni bachela na mpaka sasa hujapata mwaliko wowote, usiwaze sana, unaweza kupika chakula chako nyumbani na ukajivinjari mwenyewe.

Kama mfuko wako uko vizuri, unaweza hata kuwaita washkaji zako kufurahia sikukuu.

**Mahitaji**

Mchele, mafuta ya kupikia, viazi mviringo, maji ya moto, viungo (pilau masala, karoti, nyanya, hoho, tangawizi, vitunguu swaumu na vitunguu maji.

Nyongeza zabibu kavu, magome ya mdalasini, iriki na mashine ya kukunia viungo, sufuria na kisu.

**Namna ya kupika**

Anza kukaanga vitunguu hadi viwe vya rangi ya kahawia, ongeza karoti na kisha nyanya. Vikaange kwa muda kadhaa hadi utakapoona vimelainika kabisa.

Unaweza kuongeza viungo vingine ikiwemo vitunguu swaumu, tangawizi kiasi, magome ya mdalasini, hiriki na pilipili manga. Baada ya hapo weka nyama iliyoiva, zabibu kavu na mchele uliooshwa na viazi, kisha changanya vizuri.

Hakikisha viazi umevikata saizi ya wastani ili viive.

Ongeza maji ya moto kwenye mchanganyiko huo lakini hakikisha maji hayazidi sana kimo cha mchele ili usipate pilau bokoboko. Maji yakikauka, punguza moto wa jiko lako kisha funika pishi lako na mfuniko usioruhusu mvuke kutoroka. Unaweza kutumia foili pia.

Lipatie pishi lako dakika tano hivi kisha onja kama umeivisha. Kama ndiyo, zima jiko lako tuendelee.

Unaweza kula pilau lako kwa juisi au soda na kachumbari na kufurahia kabisa mlo wako wa sikukuu hii.

MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# KITANDA CHA CHUMA NYUMBANI NA FAIDA ZAKE

MOJA kati ya mambo muhimu katika ununuzi ambayo mtu hufanya katika nyumba yake ni kitanda kutokana na umuhimu wake hasa kwa kupumzisha mwili baada ya shughuli nyingi za kutwa nzima.

Kitanda cha chuma nacho kinapowekwa kwenye chumba nyumbani kina mvuto wake kwenye nyumba.

Mbali na kuleta mvuto kwenye chumba nyumbani, Erick Fabian ambaye ni mtengenezaji wa vitanda vya chuma katika eneo la Makonde Kinondoni Dar es Salaam anaeleza faida na hasara za kutumia kitanda hicho.

Kwa upande wa faida zake anaeleza kwamba kitanda hicho cha chuma ni imara na kina uwezo wa kudumu kwa muda mrefu.


Faida nyingine anasema kina uwezo wa kuhimili uchakavu na hakiharibiki kirahisi hata pale kinapokuwa kimetengenezwa kwa mtindo wa kubebana juu na chini.

Pia anasema kitanda hicho ni chepesi ukilinganisha na kitanda cha mbao ngumu na kwamba ni rahisi kukipangilia kwenye chumba namna unavyotaka.

Kwamba hata unapotaka kukifungua kwa ajili ya kukisafisha kwa ndani zaidi au kwa kuhamisha katika chumba kingine hakisumbui kwa sababu ni rahisi kukifungua.

Pia anasema kitanda cha chuma kina matumizi madogo ya eneo la chumba kwenye nyumba kwa sababu miguu yake ni myembamba tofauti na ilivyo kwa kitanda cha mbao.

Pia anasema kwa kawaida kitanda cha chuma kimepanda juu, hivyo



kinampa msafishaji urahisi wa kufanya usafi hadi chini ya uvungu.

Kuhusu hasara zinazotokana na kitanda hicho cha chuma kwenye nyumba, Erick anasema ni kuharibika kwa mipira inayokuwa imewekwa kwenye miguu inayokishikilia ambayo inaposagika na isipobadilishwa kwa haraka huharibu sakafu hasa pale kinaposogezwa.

Na kwamba kitanda hicho kina kawaida ya kubadilika kuendana na hali ya joto au baridi endapo chumba kikipata baridi au joto, huwa vivyo hivyo kwa kitanda kuwa na joto au baridi katika nyakati za baridi na pia kitanda hicho hushika kutu.

"Kitanda cha chuma kinaweza kisiwafae watu wa mabondeni ambao nyumba zao zinatuama maji sakafuni kwa sababu, endapo maji yakituama kwenye chumba kwa zaidi ya siku tatu upo uwezekano mkubwa wa kutoboa sakafu na kudumbukia ndani kidogokidogo, lakini pia miguu ya kitanda chake inaweza kuharibiwa na kutu,"anasema Erick.

## Yajue maua yanayovumilia jua

**Na Restuta James**

NI wazi kwamba katika ujenzi wa nyumba, kuna upande ambao utapata jua kwa muda mrefu zaidi na kuna mwingine utapata kivuli zaidi.

Hii haikuzuii kupendezesha pande zote kwa maua kama utaamua kwa kuwa zipo aina za maua zinazomudu mazingira ya kila upande; yaani jua au kivuli.

Ifuatayo ni orodha ya baadhi ya maua yanayohimili jua pale tu utakapoyatunza vizuri kwa kuhakikisha yanapata maji kila siku na mbolea mara kwa mara.

Wataalamu wa mimea wanataja yasmini kama ua linalofaa kwa upande wa nyumba ambao unapata jua muda mrefu.

Hili linatajwa kwamba linapokuwa juani na kupata maji kila siku pamoja na mbolea, utaifurahia mandhari yako kwani halikosi kijani kibichi mwaka mzima na litachanua maua yake meupe ya kuvutia.

Ua lingine ni hibiscus. Linastawi maeneo mengi kama ilivyo yasmini na linavumilia jua. Mchawi wa ua hili ni maji na mbolea; litachanua maua mwaka mzima na kama unavyofahamu, lina aina tofauti za maua kama pinki, nyekundu,bluu na mchanganyiko wa nyekundu na pinki.

Crassula ovata au jade. Hili ni ua linalotajwa kwa asili ya Afrika Mashariki na kwa sehemu linapatikana Afrika Kusini.


Ni ua linalokuwa taratibu sana lakini linaweza kuwa kama mti mdogo baada ya miaka kadhaa. Lina chanua maua meupe mwaka mzima.

Kutokana na kwamba linaweza kuwa mti mdogo mbeleni, inashauriwa usipande karibu sana na ukuta.

Ua lingine ni euphorbia trigona ambalo lina sifa moja mahsusi yaani ule uwezo wake wa kuwa na mchanganyiko wa rangi nyekundu na zambarau kwa wakati mmoja kwenye shina lake.


Upekee mwingine ni umbo lake la pembetatu, majani machache na miiba.

Garden croton. Haya yanasifika kwa upekee wake wa rangi nyingi kwenye jani moja. Halichanui maua ila uwezo wake wa kuwa na rangi nyingi kuanzia zambarau, nyekundu, nyeupe, njano nk kwenye jani moja pamoja na kuhimili jua, linanogesha nyumba zaidi.



Ili kufurahia ua hili ni muhimu uhakikishe linapata maji ya kutosha na mbolea mara kwa mara.

## KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
KITUONI
PASAKA WALEVI KAMA NYIE NI WENGI SANA...NIKIWASIMAMISHA MKIBISHA NASIMAMA BARABARANI TUONE!
NNAIMANI USHAANDIKA WOSIA
AFANDE ZILE NDUNDI HATUJAPANGA NA HUYU BWEGE NI MIPOMBE YA KILISIMASI TU!
UKITAKA KUJUA KAMA TUMELEWA MSIKIE HUYU MBWISI PASAKA KASEMA KILISIMASI!
MUSINIKOMFYUZI NIKAKORAPUTI NIKAIKORAPUSHENI SIMAMENI MUNIPE 'SHOO KIDOGO' MUPEANE NDONGA
NIMEFOSI KULEWA 'NIMESHOBOKEA' ZA KIENYEJI SIJAULIZA ILI NITAMBE SIKUKUU KUMBE NIMEGEUKA 'SEFU KONTENA' CHOO NDANI
KILABUNI
POMBE GANI 'MENI ALONI' MFUKO UMENIWEKA KOLOKOLONI NISIMWAGE LAZI NA WAREMBO PASAKA YOTE HII
KAJUA NIPO MFUNGONI ANANIALIKAJE BUFEE LA PASAKA LILONAWILI?
HAPO NDIPO UTAKAPOJUA KUMILIKI HOTIPOTI' SIO HANASA NDIO MAANA KWA MASELA HALIKOSI HA HA HAAA!
DUH!
TUKANYWE KISTAARABU KILA MMOJA AJUE WAJIBU WAKE KATIKA KUAGIZA NA KULIPA
'HIVI USTAARABU NA ULEVI WA POMBE ZA SIKUKUU VINAKAA PAMOJA VINAELEWANA?
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...RIZIKI YA MWENZAKO NI KAMA UPEPO HUWEZI KUIZUIA UTAICHELEWESHA...

# Waliomuua balozi wafungwa maisha

**KINSHASA,** DRC

MAHAKAMA ya kijeshi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, imewahukumu wanaume sita kifungo cha maisha jela kwa kumuua balozi wa Italia mwaka 2021.

Balozi Luca Attanasio, aliuawa wakati msafara wa Umoja wa Mataifa ulipovamiwa katika eneo la mashariki mwa nchi hiyo lenye machafuko.

Watu wengine waliofariki katika tukio hilo ni dereva Mustapha Milambo na ofisa wa polisi wa Italia Vittorio Lacovacci.

Awali, waendesha mashtaka waliomba hukumu ya kifo kwa washtakiwa hao na kuwaita wanachama wa genge la uhalifu.

Washtakiwa hao ambao walikamatwa Januari mwaka jana, walikana mashtaka hayo huku mawakili wao wakisema watakata rufaa dhidi ya hukumu hiyo.

**DW**

# Israel, Palestina zatakiwa kuacha ghasia

**MOSCOW,** RUSSIA

NCHI ya Russia imewataka Israeli na Wapalestina kuzuia kuongezeka kwa ghasia na kutafuta maelewano.

Wito huo ulitolewa baada ya Israel kuishambulia Lebanon na Ukanda wa Gaza kujibu mashambulizi ya roketi dhidi ya ardhi yake.

Wanawake wawili wa Israel waliuawa, na mama yao alijeruhiwa vibaya katika shambulio lilofanyika Ukingo wa Magharibi unaokaliwa, baada ya mashambulio hayo.

"Tunatoa wito kwa pande zinazohusika kujiepusha na makabiliano yoyote na kuchukua hatua ili kuzuia kuongezeka kwa uhasama, kumaliza ghasia na kufikia usitishaji wa kudumu wa mapigano," Wizara ya Mambo ya Nje ya Urusi ilisema katika taarifa yake.

Israel ililenga ngome za vuguvugu la Palestina Hamas huko Gaza na Lebanon, kujibu shambulizi la makumi ya roketi dhidi ya ardhi yake.

Baada ya utulivu katika mzozo wa Israel na Palestina ulioshuhudiwa tangu kuanza kwa mfungo wa mwezi mtukufu wa ramadhani, mapigano ya yaliibuka Jumatano kati ya vikosi vya Israeli na Palestina katika msikiti wa Al-Aqsa huko Jerusalem, eneo la tatu takatifu katika Uislamu na kuchochea uhasama.

Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu alisema majeshi ya Israel yalilazimishwa kuchukua hatua ili kurejesha utulivu dhidi ya wanamgambo wenye msimamo mkali.

# China yaizingira Taiwan

**BEIJING,** CHINA

CHINA imetuma kikosi chake cha jeshi kufanya mazoezi ya kivita ya kukizingira kisiwa cha Taiwan, kwa muda wa siku tatu.

Nchi hiyo inaitazama Taiwan kama jimbo lake lililojitenga na imeitaja operesheni hiyo kama onyo kali kwa utawala wa kisiwa hicho.

Mazoezi hayo yalianza saa kadhaa baada ya Rais wa Taiwan, Tsai Ing-wen kurudi kutoka ziara ya Marekani. Wizara ya ulinzi ya Taiwan ilisema ndege 42 za kijeshi za China na meli nane zilivuka mpaka wa Taiwan baharini. Vyombo vya Habari China vilisema mazoezi hayo yataandaa doria na kusogea katika maeneo yanayokizunguka kisiwa cha Taiwan, na kutoa taswira ya kuizingira na kukitishia kisiwa hicho kinachojitawala.

Viliongeza kwamba makombora ya roketi ya masafa marefu, mifumo ya kuharibu makombora ya baharini, boti za makombora, ndege za kivita ni miongoni mwa zana zinazoshiriki katika luteka hiyo ya kijeshi. Taiwan inajitazama kama taifa huru, lenye katiba na viongozi wake. Lakini China inatazama kama sehemu ya eneo lake lililojitenga ambalo hatimaye litarudishwa chini ya udhibiti wake kwa nguvu ikibidi.

**BBC**



Kiongozi wa kanisa katoliki duniani, papa Francis akiwasalimia waumini waliojumuika katika ibada ya njia ya msalaba juzi, hata hivyo kiongozi huyo alishindwa kuhudhuria misa ya Ijumaa Kuu iliyofanyika katika kanisa la Mt. Paulo mjini Roma.
**PICHA: DW**

# Russia yapeleka zana hatari Bakmut

**WASHINGTON,** MAREKANI

TAASISI ya Utafiti wa Vita (ISW) imesema Russia imeingiza Ukraine mifumo ya silaha ambayo inakisiwa kuwa na nguvu ikifahamika kama thermobaric Sontsepek.

Mifumo hiyo hatari ilipelekwa katika ngome ya mji wa Bakhmut, hivi karibuni ikiambatana na wanajeshi wa kawaida kwa ajili ya kuimarisha vikosi vya mamluki kwa jina wagner

Bakhmut inaendelea kuwa sehemu ya mbele katika vita.

Vyombo vya habari vya Russia viliandika kwamba vikosi vya Jeshi la Ukraine vinaondoka mjini humo ili kuepuka kuzingirwa.

Lakini upande wa Ukraine umekanusha habari hizo na kueleza jeshi bado linashikilia ulinzi katika mji huo na Bakhmut haiko chini ya udhibiti wa Russia.

Kulingana na ISW, vikosi vya Russia vimekuwa vikitumia silaha aina ya TOS-1A ("Sontsepek") pia mifumo ya silaha za thermobaric katika eneo la Bakhmut.

Katika taarifa yao ya kila siku, wataalamu walizingatia sana uchambuzi wa hali katika mji huo wa mashariki mwa Ukraine.

Kulingana na ISW, mifumo ya silaha za thermobaric ya TOS-1A huenda ilipokelewa na vikosi vya anga vya Russia na Idara za 76 na 106 za Walinzi wa Ndege.

Vikosi vya Jeshi la Ukraine havikuweza kuthibitisha habari hiyo, lakini vilifafanua kuwa data kama hizo zinaweza kupatikana na watalaam kupitia njia za ziada za ufuatiliaji, hasa, picha za setilaiti.

Wakati huo huo, uimarishaji wa vikosi vya Russia huko Bakhmut kwa kuongeza askari wa doria umefanyika.

"Warussia wanaimarisha vikosi vyao huko Bakhmut peke yao. Wagner ilijaribu kutumia nguvu ya ukiritimba katika mwelekeo huu, hata ilijaribu kuunda vitengo vyao vya hewa na silaha. Hata hivyo, kutokana na hasara kubwa, tumegundua katika wiki za hivi karibuni wanaimarisha vikosi vyao na vikosi vya jeshi la kawaida la Russia, ikiwa ni pamoja na wanajeshi wa angani," alisema Serhiy Cherevatyi, msemaji wa kundi la vikosi vya Mashariki, aliiambia BBC.

Kulingana na ISW, video za kijiolojia zinathibitisha kuwa wanajeshi wa Russia wamesonga mbele kaskazini mwa Bakhmut, kaskazini mwa kijiji cha Khromovo, kilomita 2 kutoka mji huo, na kaskazini mashariki mwa Orikhovo-Vasylivka, umbali wa kilomita 11.

Picha nyingine zinaonyesha vikosi vya Ukraine vikisonga mbele kwenye maeneo ya magharibi mwa Novobakhmutivka, kaskazini mwa Avdiivka.

Hata hivyo, bado haijulikani ikiwa Vikosi vya Jeshi la Ukraine vinashikilia nafasi ya ukubwa upi katika maeneo hayo.

**BBC**

MAKALA

# WARAKA KWA WANAHABARI NCHINI



Na Magabilo Masambu

AWALI ya yote nipende kutumia nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuru wanahabari wenzangu popote mlipo kwa kazi nzuri ambayo tumekuwa tukiifanya katika kuhabarisha, kufurahisha, kuelimisha na hasa kuisemea jamii kwa mamlaka zinazohusika.

Leo nimeona tuzungumze kidogo kupitia ukurasa huu, inawezekana sisi wenyewe tunaoandika habari na kuzitangaza lakini tumekuwa si wasomaji wa habari au wasikilizaji na watazamaji wa habari zetu wenyewe.

Kwa hiyo kuna uwezekano wa kuwa kama wapishi wa chakula ambao mara nyingi hushibia jikoni kwa kukinai chakula hata kama hawakula kwa sababu wanakiona muda wote wa maandalizi yake.

Taaluma ya habari ni kama taaluma ya siasa au baadhi ya taaluma zingine ambazo zinafanywa na watu waliozisomea na wale wasiyozisomea kwa maana ya kutumia vipawa walivyojaaliwa na Mwenyezi Mungu. Kuna watu wanasoma sayansi ya siasa, (political science) na kuna watu hawajawahi kuliona darasa, lakini wanapokuwa kwenye uwanja wa siasa huwezi kujua nani msomi au nani hajasoma kwa sababu kuna watu wamezaliwa wakiwa wanasiasa na wengine wana vyeti. Ndivyo ilivyo hata kwenye habari na baadhi ya kada.

Kwenye taaluma ya habari kama tunavyofahamu, kuna mambo yanafanyika taarifa fulani kuwa habari kwa maana nyingine si kila taarifa ni habari mpaka kuwapo vitu kadhaa ili kuwa habari. Moja ya vitu hivyo, ambacho ndicho kimenifanya niandike waraka huu ni juu ya watu maarufu (prominent figures).

Ni ukweli kwamba watu maarufu katika jamii wanatengeneza habari. Hilo halina ubishi tunakubaliana. Ni ukweli kwamba pamoja na kuhabarisha umma, tunahitaji vyombo vya habari kujiendesha kwa maana ya kutengeneza habari ambazo zinauza. Kama ni magazeti yauzike, kama ni redio zisikilizwe na kama ni runinga zitazamwe zaidi.

Tatizo langu kubwa ni juu ya kuwatengeneza hawa watu maarufu. Wakati watu hawa hawajulikani, huwa hatuhangaiki kuwafanya wajulikane. Lakini wakishajulikana kila mtu anapenda kuwatumia ili auze habari.

Jambo hili ni kama lilivyo jambo la maendeleo kwamba kila mtu anataka aishi vizuri, lakini si kila mtu anapenda kuhangaika ili aishi vizuri kwa sababu njia ya kuelekea mafanikio ni njia iliyojaa miiba na vurugu nyingi sana. Ndiyo maana wengine wakiona wanachelewa kufika, wanatumia njia za mkato na zenye madhara makubwa kwao.

Sisi wanahabari tumejenga utamaduni wa kuwatumia hawa watu maarufu katika shughuli zetu lakini hatujajikita katika kuwatafuta na kuwajenga kutokea chini. Pengine naweza kuulizwa kama hatuwapi nafasi wanajulikanaje? Ukitaka kujua jibu ya swali hili, waulize watu maarufu kadhaa wakupe hisitoria ya namna walivyopata nafasi ya kuonekana au kuandikwa utachoka.

Ninao ushahidi wa baadhi ya watu maarufu ambao wamewahi kukataliwa kufanya mazungumzo kwenye vyombo vya habari kwa kigezo kuwa wao si maarufu na hawajulikani lakini baada ya utumia njia nyingine wakajulikana. Vyombo vile vile vilivyowakataa, vinataka kuwatumia tena kuuza habari zao. Hii ni ajabu sana.

Sisi kama wanahabari tunao wajibu wa kuwafanya wasiyojulikana wakajulikana, halafu tunauza habari zetu kwa kuwategemea waliyo maarufu tu, maana wanazeeka tusipowatengeneza wengine kwa kasi, kuna siku tutakosa watu wa kuuza habari zetu. Tena eti wakija kwetu hawajulikani, tunawaambia kwamba kama wana mambo yao wanataka jamii iwaone, walipie vipindi ili waonekane!

Lakini tukiwatazama unakuta ni watu wasiyo na fedha, ila fedha zao ziko kwenye mawazo na maono waliyo nayo vichwani tuwape nafasi ya kuonyesha uwezo wao, kesho na kesho kutwa wakiwa maarufu tutakuwa na cha kujisifu na kwamba tumetoa mchango mkubwa katika umaarufu wao.

Fedha ni muhimu sana katika maisha, lakini haiwezi kuwa kila kitu, tukiweka fedha mbele tutazipata kwa wakati huu lakini tutazikosa, siku zijazo tujifunze kutengeneza fedha na siyo kutafuta fedha, anayetafuta fedha anaweza kuzipata leo na kesho zikaisha, lakini anayetengeneza fedha anaweza asizipate leo ila akizipata kesho zitadumu zaidi muda mrefu.

Kwenye jamii wako watu au vijana wao uwezo mkubwa wa mambo mbalimbali. Wengine ni waandishi wazuri hawajapata nafasi ya kuonyesha uandishi wao.

Wengine ni watangazaji wazuri, wengine katika sanaa za maigizo na kadhalika. wengine ni wanasiasa wazuri lakini hawapati nafasi kwa sababu tunataka majina makubwa watu watazame. Ndiyo, lakini kuna haja ya kuwa na mkakati wa kunoa wengine walioko chini huku.

Nawashauri wale wanaoona wana uwezo wa kipekee katika maeneo mbalimbali. Nenda popote kilipo chombo cha habari eleza nini unajua. Kama ni kuchambua siasa waambie na kama ni kuandika sema na hapa kama mwanahabri mwenzangu una wasiwasi na mtu. hebu kaa naye pembeni msikilize ana nini kichwani akiwa na mambo ya maana mpe nafasi.

Hii ni kwa sababu ni jambo la maana sana kuwa na vyanzo vingi vya habari kuliko watu wale wale ulio nao. Noa watu wako kuwa daraja la watu kupita. Huwezi kujua unaweza kutengeneza maisha ya mtu kesho akawa Rais wa nchi hii hajakukumbuka tu.

Pamoja na kwamba tunahitaji kujiendesha kibiashara, tutazame na eneo hili la kutengeneza kina Jaji Warioba, Jenerali Ulimwengu, Butiku, Zitto na wengine kadha wa kadha.

Nimshukuru sana Ramadhani Mvumgi alipokuwa Star TV na sasa yuko Azam TV kwa kuniibua kutokea huko vichakani. Vilevile Nipashe, mwanga wa jamii, kwa kuchapa makala yangu ya kwanza kabisa nikiwa si mwanahabari.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**DAR ES SALAAM-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Waliowasomesha wachumba wao wakawasaliti wanavyolia



Na Adam Fungamwango

INATIA simanzi na uchungu mkubwa kwenye dunia hii ambayo haina wema. Mtu anajitolea anafanya kila kitu kumfanya mwenzake awe na furaha, lakini malipo yake hayalingani hata chembe na alichofanya.

Nadhani utakuwa umewahi kusikia habari nyingi za wanaume wanaowasomesha wapenzi na wachumba zao, lakini baadaye wanageukwa.

Wapo wanaume wanawasomesha wapenzi na wachumba zao kwa makubalino ya kuoana baadaye na matumaini ya kuendelea na uhusiano wa kimapenzi lakini baadaye hali inakuwa tofauti.

Tumeona, baadhi ya wanawake wanakiuka makubaliano na kuamua kuanza maisha yao mengine baada ya kukutana na mazingira na watu tofauti chuoni au huko wanakosoma.

Mara nyingi wanaoamua kuwasomesha wapenzi, wao wenyewe wanakuwa hawana elimu kubwa, lakini wanaamua kuwasomesha au kwenda kupata elimu ambayo ni kubwa zaidi yao.

Ninachokiamini ni kwamba mwanamke mwanzo anakuwa hana wazo hilo la kumsaliti anayemsomesha, lakini tatizo kubwa linakuwa mazingira anayokutana nayo huko anakokwenda na watu anaokutana nao.

Msichana anatoka mtaani ambako alikuwa na mchumba wake mwenye elimu ya kawaida, anakwenda kukutana na mazingira mengine ya chuo na watu wenye elimu kubwa, kipato, na tabia tofauti, hivyo wanambadilisha au kubadilika mwenyewe kutokana na mtazamo wake.

Anagundua kuwa kumbe mpenzi wake hana elimu kama aliyowakuta chuoni, ni bora awe na watu wenye uwezo mkubwa wa kuelimu na kipato pia kwani anakuta pia huko.

Zipo pia tabia ya baadhi wa wasomi wa Kiafrika, wanapoanza kuelimika, au kupata elimu hata tabia zao zinabadilika, ikiwemo hata kubadilisha wapenzi na kusaka wanaoendana nao.

Tukirudi kwenye suala ya wanaume kuwasomesha wapenzi wao halafu wakapigwa 'kibuti' lipo tangu miaka ya nyuma, lakini kwenye miaka ya karibuni limeonekana kushika kasi hasa barani Afrika.

Tumesoma kwenye magazeti na mitandao ya kijamii, baadhi ya wanaume wanaoshindwa kuhimili presha za kugeukwa na kuamua kulipa kisasi kwa kuua au kujiua wenyewe, lakini huu siyo ufumbuzi.

Kinachotakiwa sasa ni kwa wanaume kutafuta ufumbuzi wa hili, labda waanze kwanza kufunga ndoa na wanawake hao halafu baadye ndiyo wawasomeshe.

Ingawa bado moja kwa moja si ufumbuzi wa asilimia 100 kwa sababu hata mke anaweza kukusaliti, lakini ni nadra sana kwani atakuwa anahofia atachukuliwaje na jamii, hasa ndugu za pande zote mbili.

Wanamuziki hawakuwa nyuma kuangalia eneo hilo tata ambapo wametunga nyimbo nyingi zinazohusiana na jambo hilo.

DDC Mlimani Park Orchestra, mwanzoni kabisa mwa miaka ya 1990 walifyatua wimbo kuitwao 'Mchumba Wangu', ukizungumzia kisa kama hicho.

"Ni nani eee aliyemdanganya mchumba wangu, najionea huruma, kwa kuwa mimi nilimuahidi tutafunga ndoa tuishi pamoja kama mume na mke, na pia mimi nilijitolea kwa gharama zote za kumsomesha, yeye akayapuuza.

"Sikufikiria, nilivyompenda yeye, ninasikitika, mchumba hanitaki tena. Sikufikiria, nilivyompenda yeye, ninasikitika, mchumba hanitaki tena. Nilimgharamia kumsomesha Chuo Kikuu na huko Ulaya, Nilimgharamia kumsomesha Chuo Kikuu na huko Ulaya, sikuamini macho yangu nilipopata barua, ilitoka kwa mchumba wangu pamoja na picha, ikionyesha siku alipofunga ndoa na bwana wa kizungu

Ohohohohohohoho mwana mama, ohohohohoho, bwana bibi ee, kweli nakuwaza usiku kucha silali nikikufikiria wewe nitafanya nini ee, kweli nakuwaza usiku kucha silali nikikufikiria wewe nitafanya nini miee o."

Katikati ya miaka ya 1990 nchini Kenya, mwanamuziki Freshley Mwamburi alitoa kibao maarufu nchini Kenya hadi leo hii kinachoitwa 'Stella Wangu', ambacho huwa kinaadhimishwa kila mwaka Mei 17. Mashairi yake ni haya hapa.

"Nilikuwa na mchumba wangu, tulipendana kama nyama choma, alibahatika kwenda ng'ambo, Chuo Kikuu kwenda kusoma miaka mitatu kule Japan kusomea udaktari, Stella wangu ee.

"Nilivyompenda Stella jamani nikajitolea kwa roho moja, nikauza shamba langu sababu yake yeye, nikauza gari langu, nikauza ng'ombe na mbuzi sababu yake yeye ili apate nauli ya ndege na pesa zingine za matumizi, huko Japan.

Ilikuwa tarehe 17 mwezi wa tano, mwaka 1992, ndiyo ilikuwa tarehe kamili ya Stella kurudi Kenya, Nilikwenda uwanja wa ndege kwenda kumlaki Stella, nilikua na anko Kilinda uwanja wa ndege

Nilikuwa Baziri Mwakomba na mkewe na watoto wake, nilikua anko Mshomba, nilikua na ndugu Hafidh mtoto wa Mombasa, ghafla ndege lipotua uwanajani tuliona vituko, Stella alishuka amebeba mtoto mikononi, nyuma yake mchumba wake mfupi, futi nne Mjapani, nilisikitika ndani ya moyo nikakosa la kufanya, nilitamani nilie kikamba lakini sikijui ilibidi nilie Kijaluo, 'angatima ngo wachoa', Freshley.

Nilitamani nilie Kihindi, lakini sikijui, ilibidi nilie Kitaita lugha ya baba na mama, 'weke mwana ibonye wada', Freshley."


**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

MIEZI miwili tu baada ya ndoa, Husna anapigiwa simu ya mtu asiyemfahamu. Haikuwa simu ya heri. Ni simu ya mtu anayeonekana amedhamiria. Amedhamiria kufanya kitu alichokikusudia. Kwenye maisha ya ndoa aliambiwa yatakuwa ya shida na raha, lakini kwake haikuwa mapema kiasi hicho. Alihisi sasa hakuingia kwenye ndoa aliyoikusudia bali ni ndoa ndoana.Ni nani aliyempigia simu Husna? Alitaka nini? Lengo lake hasa ni nini? Ni kweli alichokusudia mpiga simu ndicho alichokihitaji ili kuvuruga ndoa hiyo? Nenda hatua moja moja kwa kusoma kila nakala ya toleo la Nipashe ili upate ukweli mzima wa kisa hiki cha utata, kusisimua, kusikitisha na chenye mafunzo makubwa kwa jamii na wanandoa wote.

# Simu ya Sumu-5

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**




ATAKUWA ni Ziada." Akajisemea kimoyomoyo. Ndiyo, Ziada ndiye mmoja kati ya wapenzi wake ambaye alikuwa akipinga kwa nguvu zote asioe, badala yake ikiwezekana amuoe yeye.

"Ananitafutia nini huyu mwanamke? Si tumeshakubaliana mimi naoa na yeye akaniambia keshapata mchumba anataka aolewe?" Ni maswali aliyokuwa anajiuliza mwenyewe Dan kichwani.

Akili yake ilitua kwa mwanamke huyo kwa sababu yeye ndiye alikuwa akimpenda zaidi kwa dhati ya moyo wake, kuliko wanawake zake wengine ambao aliona kabisa walikuwa wanampendea pesa na si kingine. Na ndiye mwanamke pekee kati ya wapenzi wake ambao hakuja kwenye harusi yake kutokana na kuumizwa na hilo. Wengine walikubali yaishe na kuwa msitari wa mbele kwenye sherehe za harusi. Walicheza sana muziki, wakimwita Husna wifi. Siyo kwamba walikuwa wanajuana, ila kila mmoja alikuja kivyake. Ni Dan pekee ndiyo aliyekuwa anawafahamu wapenzi wake waliofika kwenye sherehe za harusi yake baada ya kukaa nao mmoja mmoja kikao kukubaliana kuwa sasa mapenzi yameisha na anafungua ukurasa mpya kwa kufunga ndoa. Ingawa kila mmoja alimuuliza kwa nini asingemuoa yeye, lakini mwishowe walisalimu amri na kuheshimu maamuzi yake. Kila mmoja aliahidi atafika kwenye harusi kwa moyo mweupe na kuanzia sasa waitane kaka na dada. Kwa Ziada ilikuwa ngumu sana. Alilia na kudai amedhulumiwa penzi.

"Ndiyo kaamua kunifanyia hivi? Atanitambua."

****************************************

"Mke wangu amerudi kwao!"

"Ina maana umempa talaka?"

"Hapana kaka, ameondoka tu mwenyewe kwa hasira."

Okay, kwa jinsi alivyokuja hapa, hata mimi nilijua tu mwisho wake utakuwa hivyo, ila nilikuwa na wasiwasi kuwa na wewe unaweza kuingia kwenye mkumbo ule ukampa talaka."

"Hapana kaka Belo."

Yalikuwa mazungumzo ya ndugu wawili, Dan na kaka yake Belo. Ngoma ilikuwa nzito kwa Dan. Kumshawishi mkewe asiondoke ilishindikana, Husna alikusanya kilicho chake na kuondoka. Hakwenda Mwanza kwa mama yake mzazi. Alikwenda Mburahati kwa mama yake mdogo aliyemlea tangu sekondari hadi alipomaliza kidato cha nne, kabla ya kumsaidia kazi za mama lishe, hatimaye kuonekana kwenye macho ya Dan, kabla ya kumuoa.

**Alikwenda Mburahati kwa mama yake mdogo aliyemlea tangu sekondari hadi alipomaliza kidato cha nne, kabla ya kumsaidia kazi za mama lishe, hatimaye kuonekana kwenye macho ya Dan, kabla ya kumuoa.**

"Enhe, wewe Dan ni mdogo wangu, niambie ukweli, imekuwaje mkeo amekuwa kwenye hali ile? Hasira si hasira, kichaa si kichaa, alivyokuja hapa kusema kweli ilikuwa inasikitisha. Amekuja hapa kama kichaa, kila mtu akawa anamshangaa, lakini maneno aliyoongea hapa yanafikirisha kusema kweli.

Aliongea maneno ambayo yanaonekana ana uhakika nayo, wala si ya kumsikia mtu, hivi kweli una mwanamke nje? Na huko Zanzibar ulikokwenda ulikuwa naye?" Belo alimuuliza mdogo wake na kumtazama usoni.

"Wewe ni kaka yangu, siwezi kukuficha chochote, ukweli kwa sasa sina mwanamke yeyote. Mwanzo huko nyuma nilikuwa nao, lakini baada ya kuoa wote niliwapiga chini.

Huko Zanzibar nilikwenda kikazi. Kwanza hiyo semina tuliyokuwa nayo huo muda wa kufanya upuuzi huo utaupata wapi? Ukweli kaka hata wewe fikiria, afadhali labda ndoa ingekuwa ina miaka mitatu minne, watu wanaweza kufikiria hivyo, miezi miwili mimi niwe nimeshafanya vitu vya namna hiyo kweli?"

"Hata mimi nashangaa."

"Sikiliza kaka Belo, mimi kabla ya kumuoa huyu binti nilikuwa na wanawake kadhaa, lakini wote nimeshaachana nao, nimeanza maisha mapya, lakini hili lililotokea hata mimi nimesikitisha sana, ila kuna msichana mmoja anaitwa Ziada. Huyu ndiyo nina wasiwasi naye."

"Kwa nini huyu ndiye una wasiwasi naye?"

"Huyu hakuonekana kuridhika mimi kuoa, nina uhakika ndiye aliyempigia simu na kumtolea maneno ya kashfa mke wangu."

"Siyo maneno ya kashfa na fedhuli tu, pia akamwambia eti sisi ndugu zako tunamfahamu yeye huyo na si huyu mwanamke uliyemuoa kwa ndoa, ni mchonganishi mkubwa huyo msichana. Umeshamtafuta na kuongea naye?"

"Hapana, ila nataka kesho kutwa nimfuate kwake kwa sababu nikimpigia simu hatutalitatua hili tatizo, na nikimpigia kumwambia tukutane anaweza kukataa kwa sababu anajua tayari kuna kosa amefanya.

Kwa hiyo mimi nataka nimshtukizie tu nyumbani kwake."

"Nenda kamwambie kama ndiyo alikuwa anatoa hasira zake za kutoolewa na wewe, ameharibu. Tena ameharibu kweli. Tuna kazi kubwa ya kufanya mpaka mama huyu arejee nyumbani. Na sisi pia ndugu zako tuna kazi kubwa ya kujikosha kwa shemeji yetu ili ajue hatujahusika na chochote."

Tunda na Halima nao waliingia. Kipindi kaka yao Dan amefika walikuwa sokoni, ingawa alikuwa wameshawataarifu kwa simu kuwa atafika nyumbani. Baada kumsalimia, walikwenda kuweka mifuko yao ya bidhaa walizokwenda kununua, wakarejea.

"We kaka we, kisa cha kutuletea ubaya wenzio kwa wifi yetu." Tunda alianza kama kawaida yake, huwa ana mdomo mwepesi zaidi kuliko dada yake Halima.

"We, acheni tu dada zangu, matatizo tu ya dunia."

"Ya dunia kaka, umetudhalilisha hapa mtaani kote. Miezi miwili iliyopita baadhi ya majirani zetu walitusindikiza kwenye ukumbi kwa ajili ya harusi.

Leo bi harusi tu bado harusi haijajibu anakuja hapa kutulalamikia. Anasema una mwanamke mwingine ambaye sisi tunamjua..!

"Yaani kaka wifi kaja hapa kama kichaa, nywele, nguo alizovaa, hasira na sauti kali aliyokuwa nayo, kila mtu alikuwa anatuuliza yule uendawazimu umemuanza? Sisi tukasema wala, ni wifi yetu yule. Kama una mwanamke mwingine na amejua umeharibu." Halima alimkatisha mdogo wake na kuongeza kwa upole na masikitiko."

"Kwanza samahanini sana dada zangu. Kitendo cha nyinyi kuhusishwa kuwa mnamjua mwanamke wangu na ndiye mnamtambua kuwa wifi yenu na si Husna, ni kuwakosea heshima. Na hakikubaliki mbele ya hata Mwenyezi Mungu kwa sababu Husna ni mke wangu wa ndoa. Lakini tatizo nimeshalijua kuna dada mmoja ndiye amefanya yote hayo, lakini nitakwenda kuyamaliza."

"Kaka twende wote tukamchambe maana atazoea siku nyingine, tutaenda kumsuta kwa rusha roho mdundiko nyuma..."

"Hapana Tunda, yeye mwenyewe anatosha, kwa sababu alikuwa mpenzi wake kabla, wanaweza kukaa na kuelewana yakaisha. Ukienda tena na wewe kwenda kufanya ugomvi huko, yatazidi kuwa makubwa." Belo alimkatisha Tunda.

**ITAENDELEA JUMAPILI**

BURUDANI

# HAMISA WIVU WAKE KIDONDA KISICHOPONA

MWANAMITINDO na mwanamuziki wa Bongo Fleva, Hamisa Mobetto, mefichua kwamba ana wivu wa kupindukia kiasi ambacho hatamani kuona wanawake wakimsogolea mwanamume wake.

Akizungumza na Millard Ayo, Hamisa ambaye ni mama watoto wawili, amesema endapo kutakuwa na ulazima anaweza kukubali kuolewa kwa ndoa ya wake wengi, yeye ndiye awe mke wa mwisho.

"Labda tu mimi na mke mwenzangu tupendane, kusiwe na vurugu. Niko na wivu mwingi hasa nikipenda mtu," alisema.

Amesema pamoja na kuwa na wivu mkali, lakini huwa hana tabia ya kumfuatilia mwanamume kwa kuhofia kujiumiza bila sababu.

"Hata uache simu hapo, hata tuambiane namba siri, siwezi kushika simu yako," ameongeza



# Baba Levo apasuka tuzo TMA

MWANAMUZIKI na mchekeshaji, Baba Levo, amemkabili Naibu Waziri wa Sanaa na Michezo, Mwana FA kuingilia kati sakata la tuzo za TMA, akisema kuna mambo hayako sawa katika utaratibu wa kuwapata washindi.

Baba Levo amekosoa utaratibu uliotumika kuwapata wateule, akisema haukuzingatia uhalisia na badala yake wasanii waliochaguliwa wamevurugwa kisaikolojia.

Akitoa mfano, Baba Levo amesema wimbo wa Dunia ambao ameimba Harmonize haukupaswa kuingia katika kinyang'anyiro cha mwaka huu kwani ulitoka 2021.

Katika vitu vilivyomstaajabisha ni kumuona Shilole kaingia katika kipengele cha Mwanamuziki Bora wa Kike na Ali Kiba kushindanishwa na vijana wadogo.

"Diamond aliamua kujiondoa kwa sababu hakutaka mambo kama haya, namuomba Naibu Waziri kuingilia kati kuweka



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### BELLINGHAM KUTUA PSG

KLABU ya Paris St-Germain imeongeza nguvu katika mchakato wa kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya England, Jude Bellingham, mwenye umri wa miaka 19 kutoka Borussia Dortmund msimu huu. (***SER Deportivos***)

### ZIYECHI ATAJWA PSG

PSG pia iko tayari kufufua nia yao ya kumsajili winga wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Morocco, Hakim Ziyech, mwenye umri wa miaka 30 msimu huu wa joto. (***Football Insider***)

### ANCELOTTI AKARIBIA CHELSEA

CARLO Ancelotti atazingatiwa na Chelsea kwa kipindi cha pili kama kocha wa Blueshao ikiwa Mtaliano huyo mwenye umri wa miaka 63 ataondoka Real Madrid mwishoni mwa msimu. (***ESPN***)

### AMRABAT ANUKIA UNITED

WAKALA wa Sofyan Amrabat amesema klabu yake ya Fiorentina iko tayari kusikiliza ofa msimu huu huku mezani kukiwa na ofa ya Manchester United ilitoa ofa kwa kiungo huyo wa Morocco mwenye umri wa miaka 26 ifikapo Januari. (***Sport***)

### SOLSKJAER ATAKIWA UBELGIJI

KOCHA wa zamani wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amejumuishwa katika orodha ya walioteuliwa kuwania nafasi iliyoachwa wazi na Scott Parker wa klabu ya Club Bruges ya Ubelgiji. (***Times***)

### PSG: MBAPPE HAUZWI

PARIS St-Germain imekatiza matumaini ya Real Madrid kumnunua, Kylian Mbappe, msimu huu wa joto kwa kutangaza kuwa hawatamuuza mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa mwenye umri wa miaka 24. (***Sport***)

### RAMSEY, NICE KITAELEWEKA

AARON Ramsey amecheza michezo ya kutosha kuamsha nyongeza ya mkataba wa mwaka mmoja huko Nice, lakini pande hizo mbili ziko katika mazungumzo juu ya mkataba mrefu zaidi wa kiungo huyo wa Wales mwenye umri wa miaka 32. (***L'Equipe***)

### IBRAHIMOVIC KIMEUMANA

AC Milan imweka wazi haitampa mkataba mpya mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Sweden mwenye umri wa miaka 41, Zlatan Ibrahimovic. (***FootMercato***)

### WATKINS MAMBO SAFI

ASTON Villa iko katika mazungumzo na mshambuliaji wa England, Ollie Watkins, kuhusu mkataba mpya kufuatia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 kuwa na kiwango kizuri hivi karibuni. (***Mail***)

### SLOT AITAKA SPURS

KOCHA wa Feyenoord, Arne Slot, anatajwa kuwania kibarua cha kuinoa Tottenham Hotspur msimu huu wa joto. (***Express***)

### ALLARDYCE KUTUA LEICESTER

ALIYEKUWA Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya England, Sam Allardyce, ameibuka kama mshindani wa ghafla wa kuinoa Leicester City. (***Football Insider***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA: HATIMA YETU YASHIKWA NA LIVERPOOL

## ●●● Lakini aweka wazi Arsenal ina rekodi ya kupindua meza katika viwanja...

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, ameitaka timu yake kujiweka kuelekea katika mchezo muhimu wa Ligi Kuu England dhidi ya Liverpool utakaochezwa leo, imefahamika.

**Ziara ya mwisho ya Arsenal kwenye ligi hiyo pale Anfield iliishia kwa kichapo cha mabao 4-0 ambacho kilimhusisha Arteta na Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp kurushiana maneno.**

Mchezo huo ukiwa 0-0 katika kipindi cha kwanza, Arteta na Klopp walilazimika kutenganishwa baada ya majibizano makali kufuatia faulo ya Sadio Mane dhidi ya Takehiro Tomiyasu.

Alipoulizwa kama atafanya tofauti mwishoni mwa wiki hii, Arteta alisema: "Sijui. Ningelazimika kuwa katika hali hiyo tena. Niliitikia kuwatetea wachezaji wetu kwa njia bora zaidi, lakini sipendi kujiona hivi. kwa matumaini sivyo."

Kiungo wa Arsenal, Granit Xhaka alitolewa kwa kadi nyekundu katika mchezo wao wa hivi karibuni dhidi ya Liverpool ukiwa ni wa hatua ya nusu fainali ya Kombe la EFL uliochezwa Januari, 2022 na ni uwanja ambao hawajashinda katika mashindano yoyote ndani ya dakika 90 tangu Septemba, mwaka 2012.

Alipoulizwa iwapo Arsenal watapaswa kudhibiti hisia zao, aliongeza: "Ndio. Wanajua hilo. Wanapitia hilo. Tunajua tunachopaswa kufanya. Tumecheza katika sehemu ngumu zaidi. Tulienda kwa Tottenham na kufanya kile timu ilifanya ikishinda mabao 2-0, hali haiwi ngumu zaidi kuliko hiyo.

"Ni timu kubwa inayosimamiwa na kocha mkuu na wanaunda mazingira ya kushangaza ambayo hufanya iwe ngumu sana kwa mpinzani yeyote.

"Ni sawa na kuja Emirates. Ni vigumu sana, kwa hiyo tunajua hilo na nafasi iko mbele yetu Jumapili.

"Kitu ambacho tumefanya katika miaka miwili au mitatu iliyopita ni kushinda katika maeneo ambayo timu haikufanya kwa miaka mingi."

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 544.

MECHI KALI
LIVERPOOL
VERSUS
ARSENAL
1 | 2.58
X | 3.40
2 | 2.45

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KOMPANY AFANIKIWA KUIREJESHA BURNLEY EPL



**LONDON,** England

KLABU ya Burnley imerejea haraka katika Ligi Kuu England (EPL), baada ya ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Middlesbrough katika mechi iliyochezwa juzi.

Middlesbrough imerejea katika EPL zikiwa zimesalia mechi saba kabla ya msimu kumalizika kutokana na kuongoza kwa tofauti ya pointi 11 kileleni mwa msimamo wa Ligi ya Championship.

Kupandishwa kwa timu hiyo kunakuja katika msimu wa kwanza wa nahodha huyo wa zamani wa Manchester City kwenye klabu hiyo baada ya kuchukua nafasi ya ukocha msimu uliopita wa joto.

Sare ya 0-0 kati ya wenzao wanaowania kupandishwa daraja, Luton Town na Millwall mapema juzi ilimaanisha ushindi dhidi ya Middlesbrough ungeifanya Burnley kupanda daraja.

Ashley Barnes aliweka Lancashire kwenye njia ya kuibuka na ushindi mnono kwa bao la kwanza dakika ya 12 huku penalti wa Chuba Akpom ya kusawazisha dakika tatu baada ya kipindi cha mapumziko ilionekana kama ingechelewesha sherehe za Burnley.

Hata hivyo, Connor Roberts aliwaweka vinara wa hao Championship mbele katikati ya kipindi cha pili na kuwahakikisha nafasi ya kupanda Ligi Kuu England.

Kikosi hicho cha Kompany kilianza msimu mgumu wa 2022-23 kwa kushinda mara moja pekee katika mechi tano za mwanzo baada ya kushushwa daraja.

Burnley wana pointi 87 na watamenyana na Sheffield United walio nafasi ya pili Jumatatu

# *Chelsea yafikiria kumrejesha Ancelotti*



**LONDON,** England

CARLO Ancelotti atafikiriwa kurejea Chelsea kwa kipindi cha pili kama kocha Stamford Bridge iwapo Kocha huyo wa Real Madrid ataondoka Santiago Bernabeu mwishoni mwa msimu huu, vyanzo vimeiambia ESPN.

Alhamisi Chelsea ilimtangaza mchezaji na kocha wa zamani, Frank Lampard kuchukua usukani kwa muda uliosalia wa msimu baada ya kumfukuza Graham Potter Jumapili iliyopita akihudumu klabuni hapo kwa miezi saba.

Vyanzo vimeiambia ESPN wamiliki wa Chelsea wanafikiria kama wagombea saba kuwa makocha wa kudumu wa kilabu, akiwemo Julian Nagelsmann, Luis Enrique na Mauricio Pochettino na Ancelotti pia yuko kwenye mfumo kwa sababu ya kutokuwa na uhakika juu ya mustakabali wake na Madrid.

Ancelotti, ambaye alishinda Ligi Kuu England na Kombe la FA mara mbili mnamo 2009-10 katika kipindi chake cha miaka miwili kama kocha wa Chelsea, anajiandaa kumenyana na klabu yake ya zamani katika mechi ya mkondo wa kwanza wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya jijini Madrid, Jumatano.

Vyanzo vya karibu na Ancelotti vimeiambia ESPN kocha huyo aliyeshinda mara nne Ligi ya Mabingwa Ulaya anakubali yuko kwenye shinikizo huko Madrid na nafasi yake itakuwa hatarini ikiwa atashindwa kutwaa taji lingine la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu baada ya kuiongoza klabu hiyo ya Hispania kutwaa ubingwa huo kwa rekodi ya 14 msimu uliopita.

HABARI MICHEZO


,830,140 JACKPOT

Lorem ipsum

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 12/04/23 | 22:00 | AC Milan vs Napoli | 2.64 | 3.08 | 2.59 |
| 02. 12/04/23 | 22:30 | San Lorenzo vs Boca Juniors | 2.75 | 2.65 | 2.49 |
| 03. 12/04/23 | 23:30 | Union Magdalena SM vs Deportivo Pereira | 2.23 | 2.95 | 3.21 |
| 04. 13/04/23 | 01:00 | Coritiba vs Sport Recife | 2.20 | 3.15 | 3.05 |
| 05. 13/04/23 | 01:00 | Belgrano Cordoba vs Huracan | 2.86 | 2.75 | 2.59 |
| 06. 13/04/23 | 03:30 | Rosario Central vs Independiente | 2.49 | 2.65 | 2.75 |
| 07. 13/04/23 | 03:30 | Estudiantes LP vs Atletico Tucuman | 2.20 | 2.91 | 3.32 |
| 08. 13/04/23 | 05:05 | Correcaminos Uat vs Club Celaya | 2.57 | 3.07 | 2.60 |
| 09. 13/04/23 | 19:45 | Feyenoord vs Roma | 2.24 | 3.14 | 3.19 |
| 10. 13/04/23 | 20:30 | Altay vs Altinordu | 2.18 | 3.12 | 3.02 |
| 11. 13/04/23 | 22:00 | Anderlecht vs AZ Alkmaar | 2.65 | 3.21 | 2.55 |
| 12. 13/04/23 | 22:30 | Colon Santa Fe vs Talleres | 2.65 | 2.80 | 2.44 |
| 13. 13/04/23 | 23:30 | Envigado FC vs Deportes Tolima | 2.75 | 2.70 | 2.46 |

MECHI ZA USHINDI

"1" – NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" – NI TIMU KUTOKA SARE
"2" – NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 09/04/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 3389 | Kashiwa Reysol vs Kashima Antlers | 3.03 | 3.28 | 2.10 |
| 13:15 | 2278 | Twente vs Cambuur | 1.25 | 5.38 | 9.36 |
| 14:00 | 3567 | Dundee Utd vs Hibernian | 3.31 | 3.31 | 2.08 |
| 14:00 | 4156 | Lyon vs Rennes | 2.11 | 3.35 | 3.15 |
| 14:00 | 4354 | Sochi vs Kryliya Sovetov | 2.02 | 3.34 | 3.39 |
| 14:00 | 4500 | Dinamo Brest vs Slavia Mozyr | 2.26 | 3.06 | 3.01 |
| 14:30 | 3535 | Anderlecht vs KVC Westerlo | 1.68 | 3.87 | 4.32 |
| 15:00 | 1938 | Buriram Utd vs Lampang | 1.11 | 6.80 | 15.46 |
| 15:00 | 5828 | Valladolid vs Mallorca | 2.42 | 2.91 | 3.01 |
| 15:30 | 2358 | RB Salzburg vs Austria Vienna | 1.30 | 4.83 | 7.61 |
| 15:30 | 3257 | Emmen vs NEC Nijmegen | 2.81 | 3.21 | 2.37 |
| 15:30 | 3604 | Rapid Vienna vs Austria Klagenfurt | 1.53 | 3.84 | 5.13 |
| 16:00 | 1335 | Leeds vs Crystal Palace | 2.06 | 3.25 | 3.35 |
| 16:00 | 1514 | Sivasspor vs Basaksehir | 2.79 | 3.00 | 2.54 |
| 16:00 | 3120 | Skovde Aik vs Jonkopings Sodra | 2.31 | 3.37 | 2.94 |
| 16:00 | 3599 | BK Hacken vs Hammarby | 1.90 | 3.50 | 3.34 |
| 16:00 | 4047 | Troyes vs Clermont Foot | 2.64 | 3.14 | 2.54 |
| 16:00 | 4611 | Reims vs Brest | 1.62 | 3.80 | 4.79 |
| 16:00 | 5626 | AC Ajaccio vs AJ Auxerre | 2.75 | 2.80 | 2.70 |
| 16:00 | 5865 | Montpellier vs Toulouse | 2.11 | 3.49 | 3.04 |
| 16:30 | 1881 | Monchengladbach vs VfL Wolfsburg | 2.32 | 3.46 | 2.71 |
| 16:30 | 5322 | CSKA Moscow vs FK Khimki | 1.25 | 5.24 | 10.27 |
| 17:00 | 2024 | Royal Antwerp vs Cercle Brugge | 1.69 | 3.82 | 4.32 |
| 17:00 | 4480 | Mlada Boleslav vs Slavia Prague | 5.70 | 4.12 | 1.51 |
| 17:15 | 3448 | Betis vs Cadiz CF | 1.62 | 3.71 | 4.91 |
| 17:45 | 2301 | Ajax vs Fortuna Sittard | 1.11 | 8.02 | 15.04 |
| 18:00 | 4359 | LASK Linz vs Sturm Graz | 3.13 | 3.29 | 2.05 |
| 18:00 | 5510 | AEK Athens vs Aris Salonica | 1.38 | 4.33 | 8.24 |
| 18:00 | 5684 | Orebro SK vs Ostersunds | 1.82 | 3.58 | 4.17 |
| 18:05 | 4922 | Nantes vs Monaco | 3.64 | 3.54 | 1.88 |
| 18:30 | 2108 | Liverpool vs Arsenal | 2.55 | 3.43 | 2.46 |
| 18:30 | 2192 | Cape Town City vs Amazulu | 1.90 | 2.85 | 3.85 |
| 18:30 | 4576 | Kalmar vs IFK Goteborg | 1.94 | 3.29 | 3.44 |
| 18:30 | 4732 | Sirius FK vs Djurgardens IF | 4.41 | 3.75 | 1.62 |
| 18:30 | 5928 | VfL Bochum vs Stuttgart | 2.90 | 3.25 | 2.28 |
| 19:00 | 2778 | FC Krasnodar vs Nizhny Novgorod | 1.62 | 3.57 | 5.25 |
| 19:30 | 3922 | Almeria vs Valencia | 2.76 | 3.21 | 2.41 |
| 19:30 | 5430 | Standard Liege vs Racing Genk | 2.62 | 3.43 | 2.43 |
| 20:00 | 1265 | Pardubice vs Sparta Prague | 6.37 | 4.78 | 1.40 |
| 20:00 | 4749 | Lokomotiv Moscow vs Zenit St Petersburg | 4.20 | 3.68 | 1.72 |
| 20:00 | 5511 | Casa Pia Atletico vs Sporting Lisbon | 7.06 | 4.34 | 1.40 |
| 20:30 | 1920 | Besiktas vs Giresunspor | 1.43 | 4.41 | 6.30 |
| 20:30 | 3015 | Hoffenheim vs Schalke 04 | 1.89 | 3.60 | 3.55 |
| 21:00 | 1674 | Panathinaikos vs Olympiakos | 2.51 | 3.12 | 2.81 |
| 21:00 | 2397 | UNAM Pumas vs San Luis | 1.97 | 3.51 | 3.56 |
| 21:00 | 3784 | Feyenoord vs Waalwick | 1.16 | 6.99 | 11.98 |
| 21:00 | 5002 | CFR Cluj vs Steaua Bucuresti | 2.21 | 3.19 | 3.08 |
| 21:45 | 2755 | Lorient vs Marseille | 4.21 | 3.91 | 1.68 |
| 22:00 | 5715 | Rayo Vallecano vs Atletico Madrid | 4.01 | 3.36 | 1.84 |
| 22:30 | 2350 | NewellS Old Boys vs Rosario Central | 2.06 | 3.06 | 3.48 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# RIVERS UNITED YATAMBA KUIFUNGA YANGA NIGERIA

**Na Saada Akida**

KIPA wa Rivers United ya Nigeria, Victor Sochima, amesema wanaujua vizuri ubora wa Yanga hasa katika safu ya ushambuliaji ambayo inaongozwa na Mkongomani Fiston Mayele na Kennedy Musonda, ambaye ni raia wa Zambia.

Rivers United itaikaribisha Yanga katika mechi ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa Aprili 23, mwaka huu kwenye Uwanja wa Adokiye Amiesimaka uliopo Port Horcout nchini Nigeria na baadaye kurudiana baada ya wiki moja kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Sochima, alisema Yanga wanatakiwa kufahamu walianza kuwafuatilia kupitia mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano mengine ya kimataifa wanayoshiriki.

Sochima alisema wachezaji wa Yanga wengi wana uzoefu hali inayofanya mechi itakayowakutanisha kutokuwa nyepesi kwa kila upande.

"Sisi tumefika hatua hii kutokana na kazi kubwa tuliyofanya kwa kutwaa ubingwa wa nchi yetu, tunawajua vizuri Yanga na wanatakiwa kutuheshimu tofauti wanavyotuchukulia," alisema golikipa huyo.

Aliongeza ugumu wa ligi ya nyumbani kwao utawasaidia kujiandaa kuwavaa Yanga na tayari wameshawapeleleza namna watakavyowakabili na hatimaye kupata ushindi.

"Unajua tunafuatilia ligi yao kwa sababu tunafahamu kuhusu Simba ni wapinzani wao wa jadi, lakini wanachotakiwa kujua haitakuwa rahisi kwa washambuliaji wao kupata nafasi ya kupata mabao kwetu kwa sababu hakuna ambacho hatujui kutoka kwao," alisema Sochima.

Aliongeza wamejipanga kuhakikisha wanapata ushindi katika mechi ya kwanza itakayocheza nyumbani kwao ili kujiweka kwenye nafasi nzuri.



Mchezaji wa tenisi, John Mpanduji, akipiga mpira kuurudisha kwa mpinzani wake (hayuko pichani), katika mazoezi yanayoendelea kwenye Uwanja wa Kijitonyama, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Mabao ya KMC kununuliwa*

**Na Mwandishi Wetu**

KUELEKEA mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Geita Gold FC, mdhamini wa KMC FC, Meridianbet, imeahidi kununua kila bao litakalofungwa na klabu hiyo ya Kinondoni kwa gharama ya Sh. 500,000 ili kuwaongezea hamasa ya kufanya vizuri.

KMC FC itaikaribisha Geita Gold FC katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano Meridianbet Tanzania, Martin Nkurlu, alisema dau hilo litapatikana endapo watafanikiwa kupata ushindi katika michezo yote ya ligi iliyosalia.

"Tunaamini fedha hizi ni zawadi ambayo itawapa motisha wachezaji kupambana kusaka matokeo bora kila watakaposhuka dimbani," alisema Nkurlu.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Thierry Hitimana, alisema motisha hiyo ni nzuri kwa wachezaji wake na itaongeza morali ya kupambana katika michezo iliyosalia ya kumalizia msimu.

"Katika maandalizi kuelekea mchezo huo, tutakuwa na mechi moja ya kirafiki na timu ya U-17 ya Azam FC, hii itasaidia kuangalia wachezaji wangu namna ya kutekeleza majukumu niliyowapa," alisema Hitimana.

KMC yenye pointi 26 iko katika nafasi ya 12 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

# Michezo

UK. 21

Nipashe

Jumapili Aprili 9, 2023




## Arteta: Hatima yetu yashikwa na Liverpool



Mshambuliaji wa Yanga, Clement Mzize (kushoto), akiwania mpira dhidi ya beki wa Geita Gold FC, Kelvin Yondani katika mechi ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la FA iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam jana usiku. Yanga ilishinda bao 1-0.**PICHA: MTANDAO**

# Yanga yatakata FA, Fountain Girls safi

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi wa mashindano ya Kombe la FA, yanga wametinga hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo baada ya kuwafunga Geita Gold bao 1-0 katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam jana usiku.

Kwa matokeo hayo, Yanga sasa itakutana na Singida Big Stars katika hatua inayofuata wakati Simba itavaana na Azam FC.

Alikuwa na straika Mkongomani, Fiston Mayele, aliyeamua mechi hiyo kwa bao la dakika 57, akiingia kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Kennedy Musonda.

Bao la Mayele lilianzia kwa Salum Aboubakar 'Sure Boy' ambaye alipiga pasi safi kwa Tuisila Kisinda, aliyekimbia kwa kasi na mpira kwenye wingi ya kushoto kabla ya kupiga krosi iliyomkuta mfungaji na aliyeusukumiza wavuni, licha ya mlinzi wa Geita Gold, Kelvin Yondani kujaribu kuuokoa.

Clement Mzize aliikosesha Yanga bao dakika ya 12, alipobaki na kipa wa Geita Gold, Athur Arakaza, lakini aliupeleka mbele zaidi kuliko makadiriko, ukawahiwa na mlinda mlango huyo.

Geita Gold ambao kwa muda wote wa mchezo walikuwa wamejazana nyuma na katikati ya uwanja, walifanya shambulizi la kwanza dakika ya 14 lililofanywa na Elius Maguri, aliyemegewa pande na Geofrey Manyasi, lakini shuti lake liliambaa pembeni badala ya kulenga lango.

Wakati huo huo, Timu ya wasichana ya Fountain Gate ya Dodoma imetwaa ubingwa wa mashindano ya Shule za Sekondari ya Afrika baada ya kuifunga Ecole Omar Ibn Khatab ya Morocco mabao 3-0 katika mechi ya fainali ya michuano hiyo iliyochezwa jana mjini Durban, Afrika Kusini.

# Simba yatangaza operesheni Aprili

## ●●● Yatamba ina jambo lake mwezi huu, moto uliowaka hautazimwa mpaka...

**Na Saada Akida**

BAADA ya kufanikiwa kusonga mbele katika mashindano ya Kombe la FA, Simba imesema itaongeza nguvu kuhakikisha inapata ushindi katika mechi zote zilizobakia katika mwezi huu ikiwamo dhidi ya watani zao, Yanga itakayochezwa Aprili 16, mwaka huu.

**Hesabu hizo za Simba pia zinajumuisha mechi ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Wydad Casablanca ya Morocco.**

Zikiwa zimepita siku mbili tangu ipokee kichapo, Ihefu FC inatarajia kuikaribisha Simba katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Highland Estates ulioko Mbarali, Mbeya na baadaye itavaana na Azam FC katika mchezo wa nusu fainali ya Kombe la FA.

Akizungumza na gazeti hili baada ya kutoa kichapo cha mabao 5-1 kwa Ihefu, Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho', amewapongeza wachezaji wake kwa kuonyesha kiwango safi katika mchezo huo ambao awali ulionekana utakuwa ni mgumu kwa pande zote mbili.

Robertimho alisema wachezaji wake walikuwa makini kuhakikisha wanatumia kila nafasi wanayopata hali iliyopelekea kuimaliza mechi hiyo katika kipindi cha kwanza kwa kupata ushindi mapema.

"Kuna baadhi ya wachezaji hawakuonekana katika mechi ya leo (juzi), nimewapumzisha kwa kuwa tuna ratiba ngumu mwezi huu, tunatakiwa kuupa umuhimu kila mchezo. Tumecheza vizuri, tumepata mabao mengi na tumeingia nusu fainali, hilo jambo zuri na muhimu, nawapongeza wachezaji wangu kazi nzuri waliyofanya.

Baada ya kupata mabao manne kipindi cha kwanza ilibidi niwapumzishe baadhi ya wachezaji na kuwaingiza vijana sababu," alisema Robertimho.

Kocha huyo aliongeza baada ya kupata matokeo mazuri wanaanza safari kuelekea Mbeya ili kuwakabili wapinzani wao katika mchezo wa Ligi Kuu ambao pia wanahitaji kuvuna pointi na wanaamini utakuwa mchezo mgumu kwa sababu wenyeji hawatakubali kupoteza kwa mara ya pili tena ndani ya siku chache.

"Sasa nguvu zetu ni mechi ya Jumatatu, mchezo huo ni muhimu kupata matokeo lakini utakuwa ni sehemu ya maandalizi ya mechi zijazo ikiwamo dhidi ya Yanga na Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema Mbrazili huyo.

Pia Robertinho aliwashukuru mashabiki waliojitokeza kwa wingi uwanjani ambao mara zote wamekuwa wakifanya hivyo na kuongeza mchango wao ni mkubwa katika kusaidia kupata matokeo mazuri.

Naye Kocha Msaidizi wa Ihefu, Zuberi Katwila, alisema hakuna anayepaswa kulaumiwa kwa matokeo waliyopata katika mechi hiyo dhidi ya Simba zaidi ya kufahamu ilitokana na makosa waliyoyafanya.

Wakati huo huo, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema malengo yao ya kutinga hatua ya hatua ya nusu fainali ya ASFC yametimia.

"Simba ikitaka jambo lake, Ihefu sio kikwazo, na sasa tunaenda kukutana nao tena nyumbani kwao, sio mechi rahisi watambue Simba tunajambo letu tunalitaka kwa huu mwezi Aprili," Ahmed aliongeza.

Kuhusu mshambuliaji wao, Jean Baleke, Ahmed alisema ni usajili bora kwa msimu huu kwa sababu siku chache alizokuwepo ndani ya Simba tayari amefunga mabao 11 katika mashindano yote.

Aliongeza kikosi chao kiliwasili salama Mbeya tayari kwa mchezo huo wa Jumatatu ambao watamkosa golikipa, Aishi Manula ambaye aliumia katika mechi ya juzi.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042